



Fuatilia mfululizo wa makala za Afcon kila Jumatatu ukurasa wa 33

Gazeti Maalum la Afcon 2027



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza katika mahojiano maalum na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Pambazuko, Peter Nyanje (kulia) na Mwandishi Mwandamizi, Andrew Msechu, yaliyofanyika nyumbani kwake Zanzibar mwishoni mwa wiki. (Picha na Fidelis Felix)

Zanzibar ni bomu

● Othman aonya inaweza kulipuka wakati wowote, hatua zikipuuzwa

Habari Uk. 6 & 7

Utajiri mawaziri wa Ruto watisha

● Vigogo wa Tanzania hali ikoje?



Habari Uk. 12



Tanzania yajizatiti kujilinda

TIMU ya maofisa waandamizi kutoka Jeshi ya Marekani itawasili nchini Tanzania kwa ajili ya mafunzo ya kuongezea ujuzi na weledi kwa wapiganaji wa Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Soma zaidi Uk. 4

INEC, Tamisemi watupiana mpira upigaji kura Ngorongoro

Uk. 8



Lissu, Mnyika, Sugu watiwa mbaroni Uk. 15

Tahariri/Katuni

Vigogo waache kusababisha foleni

HABARI kwamba misafara ya viongozi wakuu wa serikali kusimamisha shughuli za uzalishaji mali katika maeneo wanakopita, siyo ngeni na kamwe siyo uongo.

Watanzania wamekuwa mashuhuda wazuri wa kadhia hii ya kusimamishwa kwa saa kadhaa barabarani – baada ya njia kufungwa, wakisubiri mkubwa mmoja apite.

Imekuwa kawaida, kwa miaka ya hivi karibuni, wananchi kusimamishwa kwa muda mrefu barabarani ama kufunga shughuli zao kwa kuwa baadhi ya viongozi wa mamlaka na idara kadhaa za serikali wanapita; ama wakienda kazini asubuhi, ama kurudi nyumbani jioni au pengine kwenda kuhudhuria shughuli nyingine.

Hawa ni pamoja na magari ya mawaziri, manaibu wao, wakuu wa idara za usalama na wengine ambao wanakuwa wakiongozwa na magari ama pikipiki za Polisi, kuashiria kuna mkubwa anapita.

Hali hii imekuwa kero, siyo Dar es Salaam tu au kwenye miji mingine mikubwa, bali hata mikoani na wilayani. Kwamba anapopita

mkubwa, watu wananyimwa uhuru wao wa kujongea kwenda ama kutoka kwenye shughuli zao za kusaka maisha ya kila siku, kisa kuna mkubwa anapita.

Sisi tunatambua kuwa Katiba inaamrisha kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, afanye shughuli zake halali bila kubughudhiwa na yeyote, lakini anapozingwa na misafara ya viongozi, hata wale wasiohitaji kuzuia watu kuendelea na shughuli zao, inakuwa kero kubwa na uonevu.

Inawezekana Dar es Salaam ndiyo inangoza kwa kero hiyo, lakini kwanini iwe kwenye jiji hilo tu wakati wakubwa wengi wanatakiwa sasa kuwa makao makuu ya nchi, Dodoma?

Sisi katika Pambazuko tunaomba wakubwa wetu kuacha kupoteza muda wa wananchi barabarani, kisa wao wanapita.

Kama ni lazima sana wao “kuwahi,” basi Polisi washauri wakubwa hao kuchelewa kidogo kutoka nyumbani ama kuwahi kutoa kazini, ili wasilete kero zaidi ya barabarani kwani foleni zilizopo ni adha ya kutosha.



Nsekela kanisani



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akiteta jambo na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Makongo Juu, Dar es Salaam jana wakati wa kukamilisha harambee ya ujenzi wa Shule ya Jumapili. (Picha kwa hisani).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



Tanzania yajizatiti kujilinda



Komando wa Jeshi la Tanzania

Na Mwandishi WETU

TIMU ya maofisa waandamizi kutoka Jeshi ya Marekani itawasili nchini Tanzania kwa ajili ya mafunzo ya kuongezea ujuzi na weledi kwa wapiganaji wa Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Lengo kubwa la mafunzo hayo ni kuwafunza wanajeshi wa Tanzania – hasa makomandoo, mbinu za kisasa kukabiliana na magaidi.

Taarifa ambazo zimelifikia Pambazuko zinaeleza kuwa mafunzo hayo yataanza wakati wowote kuanzia sasa baada ya nchi hizo mbili kuingia mkataba wa kufanya hivyo.

Wiki iliyopita, Marekani ilikuwa na mazungumzo na Tanzania kuhusu namna nchi hiyo

tajiri kivita, inavyoweza kusaidia Tanzania kumaliza tishio la ardhi yake kushambuliwa na magaidi.

“Tunadhani kuna fursa za kuimarisha ushirikiano wetu wa kiusalama ili kusaidia kukabiliana na changamoto za kigaidi kwenye mpaka wa kusini mwa Tanzania,” alisema Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Marekani (anayehusika na siasa), John Bass, wakati akihitimisha safari ya Tanzania.

Bass, pamoja na mambo mengine, timu yake ilifanya mazungumzo na Tanzania kuhusu kuhakikisha usalama wa nchi dhidi ya magaidi na waasi kutoka nchi jirani.

Wakati wanajeshi wa Marekani wakijiandaa kuwasili, tayari wanajeshi waandamizi wa China wako kwenye mazoezi ya pamoja na wapiganaji wa JWTZ kukabili waasi wa Msumbiji kanyakaga ardhi ya Tanzania.

Baada ya wakufunzi hao kumaliza kazi yao, wenzao kutoka Marekani wataanza kufunza wapiganaji wa JWTZ namna ya kudhibiti magaidi kwa mbinu za matumizi ya teknolojia.

Hivi karibuni, wanajeshi kutoka China waliwasili Dar es Salaam, kwa meli za kivita zilizoitia nanga Bandari ya Dar es Salaam.

Mazoezi ya China na JWTZ yanajumuisha weledi wa kupigana na kudhibiti maadui ndani ya maji na nchi kavu kwa kutumia silaha za kisasa zaidi.

Sehemu ya mpaka wa Tanzania – hasa maeeneo ya Mto Ruvuma, yanayopakana na Msumbiji, yako katika hadhari kubwa kwani ni jirani zaidi na Jimbo la Cabo Delgado, Msumbiji.

Katika jimbo hilo, ndiko kuna kambi za waasi wa ambao wanaungwa mkono na kusaidiwa na makundi ya kigaidi, likiwamo la IS. Waasi hao wamekuwa wakipigana na Jeshi la Msumbiji kwa muda mrefu sasa na kusababisha uharibifu wa mali, ulemavu wa kudumu na vifo.

Inaelezwa kuwa raia wa Msumbiji wanaofikia 4,000 wameuawa na watu 946,000 wamelazimika kuyahama makazi yao tangu mwaka 2017.

Katika kukabiliana na waasi na magaidi hao, Msumbiji imekuwa ikisaidiwa na wanajeshi kutoka vikosi vya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na wanajeshi wa Rwanda, hata hivyo, bado ni “wasumbufu.”

Fomu moja kwa Rais Samia hapana

Na Igo AI

MOJA ya maazimio ya komredi Tai - kwa mwaka huu, 2024 ilikuwa “kujifua” kwa ajili ya kugombea nafasi kubwa ya kisiasa mwakani, 2025.

Nafasi hiyo ni urais; kwamba anatamani kuwa kiongozi mkuu wa Tanzania na watu wake; lije jua, inye mvua. Lazima akomae na ahakikishe anaupata.

Hata hivyo, Tai hakutaka kuweka hadharani mipango aliyoinuia, achilia mbali maazimio yake kwa mwaka huu, lakini amesukumwa na kauli za baadhi ya viongozi wa serikali ya sasa na wale wa chama tawala; Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Sababu za kugoma kuweka maazimio yake hadharani, ni woga wa kufanyiwa fitna, dhihaka na hata figisu na watu ambao anawafahamu vilivyo; kwamba wengi wamejaa uhuni na roho mbaya.

Lakini, Mzee Tai alivyosikia kauli ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuonekana kuungwa mkono na makada kibao ndani ya chama chake, akaona asikae kimya; lolote linaweza kutokea na ndoto yake kukatizwa.

Akiwa amejiipumzisha mahala, Mzee Tai aliwasikia vigogo kadhaa wakisema kwamba wanafikiri kujiandaa kuvishawishi vikao vya wakubwa ndani ya chama chao, eti mwenyekiti wao, Rais Samia Suluhu Hassan awe mgombea pekee wa nafasi ya urais wa nchi yetu.

Eti wakubwa hao watakusanya nguvu za kuhakikisha kuwa fomu itakayotolewa ya kugombea nafasi ya urais, iwe moja tu.

Kwamba mitambo mikubwa ya kuchapisha fomu za wagombea iwashwe; utumike umeme; walipwe watendaji; zinunuliwe karatasi, halafu ichapwe fomu moja tu.

Mzee Tai kusikia hivyo, akaona haiwezekani, akaita waandishi wa habari, huku akionekana kufura na kukasirishwa na kauli za makomredi wenzake.

“Hivi hawa watu wana akili gani, nani kawatuma, mbona wanataka kugeuza chama chetu kuwa cha kidikteta, nani kawaambia mama anaogopa ushindani,” akang’aka Tai.

Hakukoma hapo, akaendelea; “yaani mambo mazuri yanayofanywa na mama yetu, leo wanajidai kumkingia kifua eti asipate ushindani ndani ya chama chetu, hawa watu ni shida sana,” Mzee Tai akatoa maneno makali mengine ambayo vyombo vya habari vimeyachuja.


Ohh! Mzee Tai akaonekana akibubujikwa chozi, akidai kwamba ni vyema mama akaachwa apambane ndani ya chama chao, ili kujua atapata nini kwenye boksi la kura wakienda kwa wanan-chi?

Mzee Tai akasema, kuchapisha fomu moja ya mgombea ni fitna kwake na kwamba ni kuitukanisha demokrasia.

Hivyo, sasa Mzee Tai ameamua kujitosa na kutangaza kuchuana na Rais Samia kwenye kinyang’anyiro cha kuongoza Tanzania kwenye uchaguzi ujao – wa 2025.

Mzee Tai anasema kuwa kuanzia sasa, anapiga kampeni kwa wajumbe wote wa CCM kukataa na kulaani kuchapishwa fomu moja ili Rais Samia apitishwe kuwa mgombea.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Zanzibar ni bomu

Na Andrew MSECHU, Unguja

ZANZIBAR inachemka! Hali ya siasa ndani ya visiwa hivyo inaleta hofu na ukimya wa Wazanzibari huenda “unazungumza zaidi.”

Hali hiyo ya kuchemka chini-chini kisiasa, inamtisha Makamu wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Othman Masoud Othman, na kui-fananisha na bomu linalosubiri kulipuka.

Othman alibainisha hayo wiki iliyopita kati ka mahojiano maalum na gazeti pa Pambazuko nyumbani kwake Chukwani, mjini Unguja.

Akifafanua, anasema utulivu unaoonekana Zanzibar hivi sasa ni ukimya ambao chini yake una maswali mengi miongoni mwa Wazanzibari, kuhusiana na mustakabali wa nchi hiyo baada ya uchaguzi mkuu mwakani, 2025.

Othman anasema baada ya ACT-Wazalendo, moja ya vyama vinavyounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kutangaza kujitoa katika kuendesha Serikali ya Zanzibar, wananchi wengi wameingi-wa hofu, ingawa hawataki kuionyesha sasa.

Mwezi Machi mwaka huu chama hicho kilitangaza nia ya kujiondoa katika umoja huo unao-husisha pia Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuto-kana na kutoridhishwa na utekelezaji wa mambo waliyokubaliana.

Othman, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa ACT-Wazalendo, aliteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya mfumo huo wa SUK.

Watu wengi wana wasiwasi kuwa kujiondoa kwa ACT -Wazalendo kwenye SUK, kunaweza kuirudisha Zanzibar kwenye siasa za chuki na uhasama kama zamani.

“Kama ukipita waulize watu wote, kila mtu sasa hivi ana wasiwasi. Pita kuanzia Maziwa Ng’ombe, nenda mpaka Chokocho, halafu anza Nungwi uende zako mpaka Mtende, kila mtu ana wasiwasi kwamba mwakani tutakuwa na uchaguzi wa nam-na gani, uchaguzi utakuwaje, kwa hiyo sasa hivi ni kimya, lakini kichoambatana na wasiwasi...”

“Kwa usahihi tunaweza kusema Zanzibar ni kama bomu linalosubiri kulipuka, ni kama tu-nashangaa kwamba watu waliojipa dhamana hii



*Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,
Othman Masoud Othman.*

na wakaona kwamba Zanzibar imetoka kwenye ile hali iliyokuwepo 2015...”

“Lakini pia na ile hali iliyokuwepo 2020, mad-hara yake tumeyaandika vizuri tumeyawasilisha kwa watu, tumewawezesha viongozi wote wawili, yaani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ku-jua hali halisi,” anasema Othman.

Othman anasema kwa upande wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan, wamemuomba akutane na viongozi, na baadhi ya waathirika waeleze dukuduku, na wasi-wasi wao.

Pia anasema wamemshirikisha Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, naye akaenda kuonana na viongozi na baadhi ya waathirika, wakamwele-za kinagaubaga athari walizozipata.

“Mimi nadhani labda kwa kuwa wengine hawa-kuona haya yaliyotokea, ila sisi tumepata fursa ya kwenda na kuona, kuwasikia watu na ukiwasikia, huwezi kuwa kiongozi na binadamu kweli halafu usitake kufanya mabadiliko ya kuwarejeshea watu ile imani,” anasema.

Othman anasema walipoingia kwenye SUK lengo lao kubwa lilikuwa kurejesha imani na ku-jenga kuaminiana, ili watu wachague viongozi wao wanaowataka kwa njia ya amani na utulivu bila udanganyifu wala kuleta yale yaliyotokea 2020.

Makamu huyo wa kwanza amesema hadi sasa hakuna hoja hata moja waliyokubaliana ambayo imefanyiwa kazi.

Inaendelea Uk. 7

Zanzibar ni bomu

Inatoka Uk. 6

Anasema mpango wa kujiengua kwenye SUK haukuwa mpango wa mtu binafsi, bali ni uamuzi wa halmashauri kuu ya chama chake ambayo iliketi Machi, 2024 na kuamua kwamba wajitoe baa-da ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa mambo waliyokubaliana na kubaini kuwa hayajatekelezwa.

“Hatuoni hata moja ambalo limetekelezwa, na kwa sababu hiyo, tuliona kuwa hakuna sababu ya kubaki kwenye Serikali ya Umoja wa Kitai-fa na zaidi kwa sababu moja ya msingi, kwamba tunapobaki kwenye SUK ni kama vile tunaambia dunia kuwa mambo yanakwenda vizuri wakati hali ni tofauti, mambo hayaendi vizuri...”

“Hadi sasa, tangu tumesema kuwa tunahitaji kujitoka, hakuna mtu mwingine yeyote aliyetupa hata rai kwamba tunafanya nini katika mazingira kama hayo...”

“Sisi tunadhani kujitoka ni njia sahihi na bora kwa sababu kwanza dunia na wananchi watajua kwamba tuna tatizo ambalo ni watu walioji-pa dhamana na mamlaka ya kuyasimamia haya,” anasema.

Anasema kwa hatua ya kutoka nje ya serikali kwanza wanakuwa na fursa kubwa zaidi ya kuyakabili hayo, kutafuta njia mbadala kwa sababu hii ilikuwa ni njia moja ambayo walihisi ndiyo sahihi.

Othman anasema kwa kuwa kwa sasa imeshindikana, siyo kwa sababu haiwezekani, bali kukoseka kwa utashi miongoni mwa viongozi.

Anasema utekelezaji wa yale yaliyokubaliwa siyo suala linalohitaji fedha nyingi kutekeleza.

“Si kitu ambacho kinahitaji mtu aende kichwa chini miguu juu, ni kitu cha uungwana tu, na maono na nia ya dhati kwamba tunahitaji kuinusuru nchi...”

Anahoji; “sasa kama haya hayawezekelezi kwa

njia hii moja, tunakwendaje tena kwenye njia hii mpaka mwisho?

“Inaonekana kuna tatizo kwenye uongozi kwa hiyo sisi tunahisi njia sahihi ni kukaa pembeni na kutafuta njia mbadala na tunajua njia yoyote ile tutakayochagua inaweza kuwa na athari yake.

“Lakini tunadhani kubaki ndani ya SUK kama haya hayajatekelezwa, basi si njia sahihi ya kuyapatia ufumbuzi yale tunayolalamikia,” anasisitiza.

Anaeleza kuwa hadi sasa wamechukua juhudi zote kama ilivyoagiza Halmashuri Kuu ya ACT – Wazalendo kwa kuonana na Rais Mwinyi, ambaye hata hivyo hajatekeleza ahadi alizowapa.

Othman anaongeza kuwa chama pia kiliwagiza waonane na Rais Samia ambaye pia wameonana naye na akawapa ahadi zake ambapo kwa sasa muda ambao alioahidi kuzitekeleza bado haujatimia.

“Tunasubiri muda utakapokamilika na kuona maendeleo ya zile hatua, ndipo uongozi wa chama uliotupa jukumu, utachukua hatua,” anafafanua.

Anasema wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wanakuwa na uchaguzi huru, wa haki na ulio salama na siyo maigizo kama ilivyokuwa mwaka 2015, wala kituko kama cha 2020.


Othman anasema kuna mambo mengi ambayo wamekuwa wakiyasukuma kwa muda wa miaka minne sasa, lakini kwa bahati mbaya hayajafanyika.

“Kwa hiyo nafasi yangu ya kwanza ni kuhakikisha kadri inayowezekeleza tunakuwa na uchaguzi wa kweli kwa sababu huo ndio msingi wa maendeleo hasa kwa Zanzibar na hata kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

“Ninaamini hilo linawezekeleza kwa sababu si jambo linalohitaji miujiza wala utaalamu ambao haupo, ni kitu ambacho kinahitaji dhamira na utashi tu wa kisiasa jambo ambalo kwa sasa bado hatulioni kwa upande wa wenzetu hawa wa CCM kwa upande huu wa Zanzibar,” anaeleza.



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



INEC, Tamisemi watupiana mpira upigaji kura Ngorongoro

Na Waandishi WETU

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), zimetupiana mpira juu ya malalamiko ya baadhi ya wakazi wa Ngorongoro kutakiwa kwenda kupiga kura Msomera.

Pambazuko limezungumza na baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa na wananchi wanaoishi Ngorongoro, wanaolalamika majina yao kwenye orodha ya wapigakura kuhamishiwa katika vituo vya upigaji kura vilivyopo Kijiji cha Msomera wilayani Handeni, Tanga.

Bila shaka hilo limetokea baada ya baadhi ya wakazi wa Ngorongoro kuhamishwa mapelelele mwaka huu kutoka eneo hilo na kupelekwa Msomera, ikiwa ni kampeni ya serikali kulinda mazingira katika hifadhi ya Bonde la Ngorongoro.

Maofisa kutoka taasisi hizo mbili za serikali kwa nyakati tofauti, juzi – Jumamosi na jana – Jumapili, walishindwa kulieleza Pambazuko juu ya sintofahamu hiyo huku kila mmoja akisema taasisi yake haihusiki na suala hilo.

Kwanza Pambazuko lilizungumza na Ofisa Habari wa INEC, Giveness Aswile, ambaye alisema kuwa tume hiyo haihusiki na malalamiko hayo kwa sababu anayepanga maeneo ya uchaguzi ni Tamisemi.

“Kuna wenzako wengi wameshanipigia simu kutaka ufafanuzi wa suala hilo, lakini nawaambia sisi hatuhusiki, bali wahusika wakuu ni Tamisemi, ambao ndiyo wanaogawa maeneo...”

“Hata hivyo, mkurugenzi wetu hapa ameshalisikia jambo hilo na anatarajia kulitolea ufafanuzi wa kina wakati wowote,” alisema Aswile.

Aidha, Pambazuko lilipompigia Ofisa Habari wa Tamisemi, Nteghenjwa Hoseah, naye akase-



Ofisa Habari wa INEC, Giveness Aswile

ma wizara haishusiki na suala hilo, kwani inafahamika kuwa taasisi inayohusika na masuala ya kupiga kura ni INEC.

“Sisi hapa hatuhusiki na suala hilo, waulize INEC ndiyo wanaojua. Lakini pia waulize hao watu wa Ngorongoro hiyo GN imetolewa na nani maana mimi sijui lolote,” alisema Hoseah.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, baadhi ya watu wanaojitambulisha kuwa wanatoka Ngorongoro, walirekodi video ambayo ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii wakieleza dhamira yao ya kuipeleka serikali mahakamani kupinga majina yao kuhamishiwa Msomera.

Katika video hiyo, baadhi ya madiwani wa Tarafa ya Ngorongoro pamoja na wananchi wengine, wanaonekana wakiilalamikia INEC, kwamba imehamishia majina yao Msomera wakati wao bado wanaishi Ngorongoro.

Aswile alipoulizwa kama ameshaona video ya wananchi hao, alikiri kuiona, lakini akamsisitiza mwandishi wetu awasiliane na Tamisemi kwa kuwa ndiyo wenye majibu sahihi na kisha akakata simu.

Diwani wa Kata ya Alaililai, huko Ngorongoro, Shutuk Kitamwasi, amesema katika video hiyo kuwa wataishtaki INEC mahakamani kwa kuwahamisha kwenye vituo vya kupiga kura kinyume cha utaratibu.

“Nasikitika kusikia kuna Tume Huru ya Uchaguzi, kwa kitendo walichokifanya Ngorongoro, hiyo siyo tume huru, Wangeendelea kuiita Tume ya Uchaguzi badala ya kuiita Tume Huru ya Uchaguzi...”

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Je, msimamo wa Chadema bado upo palepale?



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe

“KAKA, hivi Chadema watashiriki uchaguzi wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji?” aliniuliza kijana mmoja ambaye kwa ufahamu wangu ni kada wa chama hicho cha upinzani.

Nikamwambia nina majibu matatu.

Kwanza, ni kwamba sijui kama chama hicho kitashiriki au la, kwa sababu mimi siyo kiongozi wala mwanachama wa chama hicho.

Pili, ni kwamba huko nyuma, chama hicho kilitamka kuwa hakitoshiriki uchaguzi wowote ule hadi katiba mpya na tume huru ya uchaguzi vipatikane.

Nikaongezea kwamba kwa sababu katiba mpya haijapatikana, na tume huru “mpya” imebadili jina tu, yayumkinika kuhisi kuwa Chadema haitoshiriki uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba, na pengine haitoshiriki uchaguzi mkuu hapo mwakani.

Tatu, halikuwa jibu, bali swali kwa kijana huyo, kwamba kwanini aniulize mimi badala ya viongozi wa chama chake au makada wenzie?

Akanijibu kwamba anaogopa kwamba akiuliza swali kama hilo anaweza kuhisiwa vibaya na wana-Chadema wenzie.

Jibu hilo la tatu likanikumbusha angalizo lililowahi kutolewa mara kadhaa na mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe akiwataka vijana wa chama hicho kutumia lugha za kistaarabu wanapopingana na mtu wasiyeafikiana naye au hoja wasizoafikiana nao.

Na pia, juzi tu, Mbowe alitanabaisha kuwa kiongozi mwandamizi wa chama hicho, Godbless Lema anachelea kuwania uenyekiti wa Chadema kanda ya Kaskazini kwa kuhofia kutukanwa.

Japo hili linaweza kusababisha vijana wa chama hicho kutukana zaidi, ukweli mchungu ni kwamba Chadema inapaswa kuchukulia tatizo hili kama existential yaani linalotishia uhai wa chama hicho.

Kwa sababu, wakati vijana wa chama tawala, CCM wanafahamika kwa umahiri wao wa lugha zisizo za kiungwana, ikiwa ni pamoja na kutoa vitisho wakidai kuwa vyombo vya dola vipo upande wao.

Chadema na vijana wake wanapaswa kuwa kinyume kabisa na hali hiyo, kwa sababu hawawezi kutaka kuwa mbadala wa CCM, ilhali nao wana udhaifu kama huo wa CCM.

Unaweza kudhani lugha isiyo ya kiungwana ni tatizo dogo, lakini ukweli ni kwamba katika siasa, kipele kinaweza kugeuka donda-ndugu. Yaani tatizo dogo la leo, linaweza kuwa tatizo kubwa kesho.

Kwa upande mwingine, ni muhimu - siyo kwa Chadema tu, bali pia hata ACT-Wazalendo kutangaza bayana endapo watashiriki uchaguzi ujao wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji hapo Novemba, mwaka huu.

Kutangaza mapema kutawapa mwanya wana-chama na wafuasi wao, kujipanga ili kuwa tayari kwa uchaguzi ujao na siyo kuwashtukiza.


Endapo vyama hivyo vitaamua kushiriki kwenye uchaguzi na kutangaza mapema, wapigakura wao watajiweka sawa ili kuhakikisha wana-shiriki kuchagua wagombea wao ili wakawe chachu kwenye vikao vya uamuzi.

https://instagram.com/evarist_chahali



Tafakuri ya Bagonza

Demokrasia na maendeleo ni 'chanda na pete'



Mwalimu Julius Nyerere

Na Dkt. Benson BAGONZA

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa wakati wake, aliamini demokrasia ya chama kimoja ingelela maendeleo.

Alijenga hoja na kuuaminisha ulimwengu juu ya azma yake ya kujenga jamii isiyokuwa na matabaka. Mwalimu alipata upinzani wa wasomi na baadhi ya wasaidizi wake.

Wakati baadhi ya wateule wake walishindwa kuiishi hiyo falsafa ya kutokuwa na matabaka na kupenda kuabudiwa na kujilimbikizia mali.

Wasomi wachache, lakini muhimu, waliikosoa falsafa hii na kumwambia Mwalimu kuwa harakati za matabaka haziwezi kuisha kwa sababu ni za asili (Class Struggles).

Mwalimu hakulikubali hili kwa uwazi mpaka mwishoni mwa enzi yake alipokubali kuwa mfumo wa vyama vingi ulihitajika ili kuleta maendeleo hapa nchini kwa njia ya kuruhusu kwa uwazi minyukano ya kiharakati za makundi mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa Tanzania ya Mwalimu ilikuwa na matabaka mawili; wakulima na wafanyakazi.

Tanzania ya sasa tuna kundi kubwa ambalo siyo wakulima na wala siyo wafanyakazi. Kundi hili linahitaji aina ya uongozi tofauti na mtido wa uongozi tunaodai unamuiga Mwalimu. Msingi wa Mwalimu upo, lakini kuta zake zimebadilika na

isiwe aibu kukubaliana na hali hii.

Mabadiliko ya mawazo ya Mwalimu mwishoni mwa utawala wake, ni muhimu sana kuzingatiwa, kwamba, enzi hizi tulizo nazo, tuukubali mfumo wa vyama vingi na maadili yake na tuuishi kikati-ba, kimuundo na kiutendaji wa serikali zetu.

Kuukubali mfumo mpya kinadharia, huku kimatendo tukiishi kama tuko chama kimoja, tunachelewesha maendeleo kwa sababu tutake tusitake, hatuwezi kurudi nyuma kama Mwalimu alivyotunya.

Sababu nyingine nzuri ya kutuzuia kurudi nyuma katika mfumo wa chama kimoja, ni pale tunapopata ushahidi kuwa hata ndani ya vyama karibu vyote, hakuna mazingira rafiki ya kupokea na kuishi na maoni tofauti tofauti.

Watu wenye maoni tofauti ndani ya vyama karibu vyote hawatakiwi. Vyama karibu vyote vinaishi ndani ya fikra za chama kimoja ndani ya vyama vyao.

Vyama vyetu vimekuwa vya viongozi na kusifiana na kulindana ndiyo sera rasmi isiyoandikwa katika ilani za vyama.

Hali ya kuambiana ukweli kwa upendo na kuwezesha kujikosoa, haipo ndani ya vyama karibu vyote.

Kwa hili, vyama vya upinzani vinaiga mitindo fulani kutoka chama tawala -CCM, na hali kadhalika chama tawala na ukongwe wake kinaigaiga baadhi ya mambo ya vyama vya upinzani.

Hali hii inaturudisha katika mtanziko (dilemma) wa kuchagua kati ya kuwa na demokrasia au kuwa na maendeleo.

Wapo viongozi ndani ya taifa letu wanaoamini kuwa maendeleo yanaweza kuja bila kuwa na demokrasia jumuishi; yaani wao wawaletee maendeleo watu bila kuhojiwa au kukosolewa.

Kwao hawa, maendeleo ni fadhila kutoka kwa viongozi kwenda kwa wananchi na hao wananchi inabidi wakae kimya, wawe watulivu, wasifie, wafanye maombi ya kuwaombea viongozi waishi maisha marefu bila kuugua, na ndipo wawaletee maendeleo hadi nyumbani kwao.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kिलutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTagaluka

Polisi wasitie doa mfumo wa utoaji haki

IMEKUWA ni kawaida kwa Jeshi la Polisi Tanzania kukamata raia baada ya kushinda kesi mahakamani.

Hatua hii huibua maswali mengi kutoka kwa wananchi, wengi wakihoji mipaka ya mfumo wa sheria, haki za binadamu, na mipaka ya mamlaka kati ya vyombo vya dola na mahakama.

Kujirudiarudia kwa matukio haya kunaasiria upungufu katika utendaji wa Jeshi la Polisi, kwa kuonekana kuingilia heshima na uamuzi wa chombo hicho cha kutoa haki.

Kadhia hii imeonekana mara nyingi, na hata masheikh waliopo magerezani ambao wanaposhinda kesi hupelekwa tena Polisi na kulazimishwa kuomba dhamana.

Hii inaonesha kwamba uamuzi wa mahakama, ambao unapaswa kuwa na nguvu ya mwisho, hauheshimiwi.

Mahakama hufanya uamuzi wake kwa misingi ya ushahidi uliowasilishwa mbele yake. Pindi inapotoa hukumu, uamuzi wake unapaswa kuheshimiwa na vyombo vyote, ikiwa ni pamoja na Polisi.

Hata hivyo, vitendo vya Polisi kuwashikilia tena watu baada ya kushinda kesi, vinaonesha kuwa kuna ukosefu wa heshima mahakama.

Hali hii inaibua maswali kuhusu mipaka ya mamlaka ya Polisi na mahakama, na kutia doa mfumo mzima wa utoaji haki nchini.

Kwa kuweka watu gerezani kwa muda mrefu huku wakitafuta ushahidi, Polisi inaonyesha kupuuza thamani ya maisha na uhuru wa raia.

Hali ya wananchi kukamatwa, na pengine kupigwa, na kuwekwa gerezani kwa miaka mingi bila ushahidi wa kutosha na baadaye kuachiwa na Mahakama, inaweza kuwa na tafsiri mbaya.

Naweza kushauri yafuatayo; kwanza ni muhimu kutenganisha mamlaka kati ya Jeshi la Polisi na Mahakama. Mahakama zinapaswa kuwa na sauti ya mwisho katika uamuzi wa kisheria, na Polisi inapaswa kuheshimu na kutekeleza uamuzi huo bila kuingilia kati.

Jambo la pili ni lazima kuwe na mfumo wa

kuwajibisha askari polisi wanapokiuka sheria. Hii inaweza kufanyika kwa kuanzisha taasisi huru ya kusimamia utendaji wa Polisi na kuchunguza malalamiko dhidi yao.

Tatu, mafunzo ya kisheria na haki za binadamu yanapaswa kupewa askari polisi ili kuhakikisha wanatambua na kuheshimu haki za raia na uamuzi wa mahakama.

Nne, serikali inapaswa kuboresha mchakato wa kisheria kuhakikisha kwamba ushahidi unakusanywa kabla ya raia kukamatwa.

Hii itapunguza uwezekano wa kuwakamata watu bila ushahidi wa kutosha na kuwaweka gerezani kwa muda mrefu bila sababu za msingi.

Hivyo basi, ni muhimu kwa viongozi wa nchi kuchukua hatua za haraka kushughulikia tatizo hili la msingi ili kulinda haki za raia na kurejesha imani kwa mfumo wa utoaji haki kwa wananchi.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Camillus Wambura

Kenya



Baraza la Mawaziri la Rais wa Kenya, William Ruto wakiwa Ikulu, Nairobi muda mfupi baada ya kuapishwa wiki iliyopita. (Picha na Nation)

Utajiri mawaziri wa Ruto watisha

Na Julius MKAMBI

BARAZA la mawaziri wa Kenya limesheheni matajiri, huku wananchi wakihoji wamepata wapi ukwasi huo?

Wananchi wengi nchini humo, kupitia mitandao ya kijamii, sasa wanauliza; wako wapi “watoto wa mkulima” masikini kama alivyoahidi William Ruto kwa wananchi wa Kenya wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2022.

Hakuna “mtoto wa mama mboga wala dereva wa bodaboda” – ambaye ameukwaa uwaziri, hatua ambayo wanaielezea kuwa ni usaliti uliofanwya na Rais Ruto.

Wanaeleza kwamba Rais Ruto aliwasaliti mara ya kwanza alipounda baraza lake la mawaziri baada ya kuapishwa, lakini amerudia “yaleyale” ya kuwapa nafasi mawaziri wenye ukwasi mkubwa.

Ruto alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwaaminisha Wakenya kwamba uchaguzi uliopita ulikuwa kati ya wanaotoka kwenye familia tajiri, dhidi ya wanaohangaika kuweka chakula mezani – akiwamo yeye.

Alipotangaza baraza lake la kwanza la mawaziri, Wakenya walishtushwa na thamani ya utajiri wa mawaziri aliyowateua, wakihoji ipo wapi nafasi ya watoto wa ‘mama mboga na madereva wa bodaboda’.

da.’

Pamoja na kwamba Rais Ruto hakuwahi kujibu swali hilo, bado amerudia kuwasahau mama mboga na wenye bodaboda, kwani watoto wao hawakonekani katika baraza lake la pili, alilounda baada ya shinikizo la vijana wa Gen Z kupitia maandamano.

Katiba ya Kenya unawataka watu wanaoteuliwa kuwa mawaziri, kuhojiwa na bunge na kuthibitishwa kabla ya kuapa kuanza kazi.

Moja na maswali yanayoibuka wakati watu hao wakifanyiwa usaili, ni kujieleza anamiliki nini; vitu vinavyohamishika na visivyohamishika, na zaidi kutaja kiasi cha fedha alichonacho, ikiwa ni pamoja na hisa katika kampuni mbalimbali.

Katika usaili huo, walioteuliwa na rais huwatakiwi kuficha, kwani “vyombo vya usalama” hufanya kazi yake na kubaini kinachomilikiwa na wahusika kabla ya kuhojiwa na bunge.

Mali walizonazo

Imebainika kuwa Baraza la Mawaziri la Ruto ambalo liliapishwa Alhamisi iliyopita Ikulu, Nairobi linajumuisha watu ambao jumla ya thamani yao ni zaidi ya Shilingi za Kenya bilioni 14.7 (ambazo ni zaidi ya Shilingi za Tanzania bilioni 300).

Inaendelea Uk. 22

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

Lugha ni pamoja na kuitumia kwa ufasaha

WIKI iliyopita tulipata fursa kuangalia jinsi baadhi ya watu wanavyotumia lugha ya Kiswahili kiholela wakichanganya na kubadili maneno na kusababisha hatari kwa lugha hiyo adhimu, kupoteza uhalisia wake.

Baadhi ya watu waliosoma makala hiyo waliokubaliana kuwa kuna haja ya kutafuta njia za kutibu ili Kiswahili kiweze kutumika kwa ufasaha wake, kwani tatizo hilo ni hatari kwa ustawi wa lugha hiyo.

Wakati tunajadili matumizi ya irabu na konsonanti, lipo tatizo jingine linaloonekana kukua pia - la watu ambao huongea Kiswahili kwa kuchanganya na maneno ya lugha nyingine hususani Kiingereza. Kuna watu wanaita matumizi hayo 'kiswanglish'.

Kama tunataka lugha yetu ya Kiswahili ibaki na heshima yake, itafaa kabisa kuilinda kwa kuitumia katika ufasaha wake. Tunafahamu kuwa lugha hukua na kuna maneno hutolewa kutoka lugha nyingine na yakatumika katika lugha kama ilivyo katika Kiswahili maneno kama gari, baiskeli yametokana na maneno ya lugha nyingine.

Jambo linalopaswa kuangaliwa na kurekebisha ni watu wanaoamua kutumia maneno ya Kiingereza wanapozungumza Kiswahili ama kwa kuwa tu anayafahamu au kwa kudhani hana msamiati wa Kiswahili.

Unaweza kuwakuta watu wanaojua Kiingereza wanaamua kutumia maneno ya Kiingereza katikati ya sentensi za Kiswahili. Mfano mtu anajieleza, "Niko kwenye kufainalaizi kazi zangu", "siwezi kabisa kukompromaiizi hili", "tulifanya analisisi ya kutosha".

Katika matumizi haya, ni dhahiri kuwa hadhira yake itakuwa inamwelewa, lakini lugha aliyozungumza siyo sahihi.

Lakini pamoja na kutokuwa sahihi kuingea hivyo, wanaweza kuwepo watu wasiofahamu



Mvulana wa Kimasai akijifunza Kiswahili katika kijiji kimoja cha Kenya. (Picha na BBC)

wala kuelewa lugha hiyo iliyochanganywa hapo, hivyo wasiweze kabisa kupata hoja inayozungumziwa au maana ya kinachozungumziwa.

Bahati mbaya sana hali hiyo hutokea hata kwenye mikutano inayopaswa kuendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

Hali hii ilinifanya nianze kuiangalia sana kwa umakini wakati nilipokuwa nikitoa elimu ya haki za binadamu huko vijijini. Kuna wakati bila kutafakari sana kati ya uelimishaji huo unakuta mtu amesema; "in fact ukweli ni kuwa" au "By the way mna mpango gani katika hili."

Hapa walitokea watu na kuuliza maana ya maneno hayo. Sasa inapokuwa limechanganywa kabisa; "hapa itakuwa wamevayoleti sheria kabisa." Unakuta watu wanaachwa wakijiuliza maana ya hayo maneno mageni na kukosa kupata ujumbe uliokusudiwa.

Wakati mwingi haya hutokea kimazoea tu na si kwa vile mtu hajui neno la Kiswahili.

Ili kuipa lugha hii hadhi yake na kuiacha iendelee kukua vizuri, ingefaa watu kujibidiisha kuiongea kwa ufasaha na pale mtu anapoona hajui kabisa neno la Kiswahili, basi akiri kwa kutaja neno la Kiingereza.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

INEC, Tamisemi watupiana mpira...

Inatoka Uk. 8

“Hivi uhuru uko wapi, hiyo tume uhuru wake uko wapi, kama leo hii unaenda kuangalia jina lako hata hujaandikishwa Msomera, lakini linaonekana utapgia kura Msomera...”

“Yaani, wakati wewe umejiandikisha mwaka 2015 katika Kata ya Ilelai, leo unajikuta jina lako liko Msomera, sehemu ambayo wananchi wengi wa Ilelai hawajawahi kufika na wala hawana mpango wa kufika...”

“Mimi hapa nilipo sijafika Msomera na sijawahi kufika na sitahamia Msomera maisha yangu yote, sasa inakuwaje leo hii unajikuta kwamba eti jina lako liko Msomera?”

“Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) analijua hili, kwa hiyo, naomba asituone kwamba sisi siyo watoto wake kwa sababu Watanzania wote ni watoto wake kwa makabila yote 120...”

“Asitubague sisi Wamasai kwa sababu hatujalifanyia taifa hili tendo baya, bali tumekuwa tukiwalinda wanyama tofauti na makabila mengine...”

“Leo hii ukienda Kondoa, unakuta watu wanaakula ndege barabarani, lakini huku unawakuta wanyama wote utadhani Shamba la Edeni...”

“Hatuwazuii watu wanaotaka kuhamia Ngorongoro kwa hiari, ila tunaobaki nikiwamo

mimi, hatutakubaliana na suala la kunyimwa haki yetu ya msingi...”

Diwani wa Kata ya Laitole, James Molinege, naye ameonyesha msikitiko yake akisema haridhishwi na kile ambacho INEC imewafanyia.

“Hili ni jambo la uonevu, ni jambo la kusikitisha, ni jambo ambalo limetukatisha tamaa na ni jambo ambalo limekuja kutukumbusha majeraha, kwani kuna wakati tulikuwa tunasemekana sisi ni Wasudani...”

“Haya, imetoka hiyo na sasa tunaambiwa kwamba hatuwezi kupiga kura kwa sababu wameniaandikia kupiga kura katika eneo ambalo sijahamia...” ameongeza

Sabila Ngalosi ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Burati anasema; “orodha ambayo imetolewa katika vituo vya kupigia kura, Tarafa ya Ngorongoro yenye Kata 11 na vijiji 25, wananchi wake hawapo...”

“Tukajitahidi kufuatilia kwenye mifumo, tukaona majina yetu yanaonyesha tunapigia kura Msomera. Kwa mfano, mimi hapa niliposimama, inaonyesha nitapigia kura katika Sekondari ya Msomera B,” ameongeza kwa masikitiko.

Anasema serikali ilianganalie upya suala hilo wka sababu kuna watu takriban 110,000 ambao wamesalia Ngorongoro baada ya wengine kuondoka kwa hiari kwenda Msomera.



Wananchi wa Ngorongoro



Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu (aliyevaa kofia) akiwa na viongozi wenzake wa chama hicho, wakimsikiliza kamanda wa Polisi Jijini Mbeya muda mfupi kabla ya kukamatwa na jeshi hilo. (Picha na Chadema)

Lissu, Mnyika, Sugu watiwa mbaroni

Maregesi Paul na Elizabeth Hombo

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya jana liliwatia nguvuni baadhi ya viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Viongozi waliokamatwa na Polisi ni pamoja na makamu mwenyekiti (Bara), Tundu Lissu, katibu mkuu, John Mnyika, mwenyekiti wa kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, almaarufu – Sugu, pamoja na viongozi wa umoja wa vijana wa chama hicho.

Imeelezwa kuwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, akiwa ameambatana na msaidizi wake, Andrew Kantimbo, ambaye pia ni mkuu wa upelelezi wa makosa ya jinai wa mkoa huo, walifika ofisi za chama hicho kanda, wakiwahitaji viongozi wa Baraza la Vijana wa Chadema (Bavicha), lakini baada ya kuwakuta viongozi wengine, waliwachukua wote na kwenda kuwahoji Kituo cha Polisi Mbalizi, Utengule.

Viongozi hao waliwasili Mbeya jana mchana kwa ajili ya maandalizi ya kufanyika kwa kongamano na maandamano ya vijana wa chama hicho yaliyopangwa kufanyika leo.

Chadema kimethibitisha kukamatwa kwa viongozi hao na kwamba hadi Pambazuko linakwenda mitamboni – saa 5:17 usiku, walikuwa bado wakishikiliwa na Polisi.


Akizungumza na Pambazuko, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema alisema kukamatwa kwa viongozi hao ni kwenda kinyume na Katiba ya Tanzania na ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kutaka kuwepo maridhiano.

Mwenyekiti wa Taifa wa Chadema, Freeman Mbowe, mara baada ya kupata taarifa hizo, aliandika katika ukurasa wake wa mtandao wa X, akilitaka Jeshi la Polisi kuwachia viongozi hao “mara moja na bila masharti.”

“Tunalaani vikali Jeshi la Polisi kukamata viongozi wetu wakuu wa chama ikiwemo viongozi wa Bavicha...”

“Tunalaani mkakati wa msajili wa vyama vya siasa kwa kushirikiana na Polisi kuzuia kongamano la Bavicha katika kuazimisha (usahihi – kuadhimisha) Siku ya Vijana Duniani hapo kesho - J'tatu, 12 Agosti...”

Inaendelea Uk. 27



Zitto alalama kuzuiwa kuhutubia ‘wakimbizi’



Zitto Kabwe

Na Mwandishi WETU, Kigoma

KIONGOZI mstaafu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ameshutumu serikali kwa kuwazuia zaidi ya Watanzania 162,000 wanaoishi katika kambi za wakimbizi za Kanonge na Katumba kushiriki masuala ya siasa.

Alitoa malalamiko hayo wiki iliyopita wakati akihutubia mkutano wa hadhara katika Kata ya Ugala, Jimbo la Nsimbo, mkoani Katavi.

Zitto alisema kuwa alikatazwa na mamlaka za serikali kufanya mikutano ya hadhara katika makambi hayo ambako pamoja na wakimbizi, lakini kuna watu 162,000 ambao ni raia wa Tanzania.

Zitto alisema kuwa pamoja na kuwa watu hao wanaishi katika kambi za wakimbizi, lakini wana hadhi ya uraia kamili wa Tanzania wakiwa na haki ya kushiriki kwenye shughuli za siasa kama walivyo raia wengine.

Watu hao 162,000 ni miongoni mwa wakim-

bizi 200,000 waliopokelewa mwaka 1972 kutoka Burundi na waliopolekwa katika kambi za Katumba na Kanonge, wilayani humo.

Mwaka 2008 hadi 2010, serikali iliamua kutoa uraia kwa wakimbizi 162,000, lakini wa-kaendelea kuishi katika makambi hayo.

“Hawa wana haki zote zinazompasa raia wa Tanzania, ikiwamo kuchagua na kuchaguliwa, na ili wapate haki hiyo ni lazima wanasiasa tu-fike huko na kuzungumza nao,” alisema Zitto.

Zitto ameitaka Wizara ya Mambo ya Ndani kutowashikilia watu hao kama mateka, kwani wana haki zao za kiraia kama walivyo raia wengine.

Zitto alisema jambo hilo halikubaliki katika nchi ambayo watu wapo huru kwenda mahali popote ilimradi hawavunji sheria.

Alisema viongozi wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Katavi waliandika barua kwa Jeshi la Polisi kutoa taarifa ya kufanya mikutano ya hadhara katika Kambi ya Kanonge ambao walipanga kuufanya Agosti 3, mwaka huu na kujibiwa kwamba “siasa hairuhusiwi eneo hilo.”

“Wananchi wanaotambulika kuwa Watanzania kwa mujibu wa sheria za nchi katika kambi hizo, wanayo haki sawa na Watanzania wengine, hivyo kuzuia mikutano ya hadhara kufanyika eneo hilo ni kuwanyima haki yao kikatiba,” alisema Zitto.

Alieleza kwamba mwaka 2020, walifanya mkutano katika Kambi ya Katumba kumwomba kura Philip Mallack kuwa Mbunge wa Nsimbo na wananchi hao walipiga kura, hali iliyomfanya ahoji mazingira ya kutoruhusiwa mikutano katika eneo hilo hivi sasa.

“Hizi ni mbinu za washindani wetu kuwatisha wakazi wa maeneo hayo. Mimi ninawaambia waacheni wawe na uhuru wa kuchagua wamtakaye, tusiwalazimishe kwa kuwa uraia wao si fadhila kwa chama fulani,” alisisitiza Zitto.

Katika mkutano huo, Zitto alikosoa pia uamuzi wa serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuongeza maeneo ya hifadhi bila kujali ongezeko la idadi ya watu.

Alisema uamuzi huo utaongeza migogoro kati ya wananchi na serikali katika eneo hilo la Nsimbo.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (watatu kushoto) akiwa na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Pambazuko, Peter Nyanje (kulia), Mwandishi Mwandamizi, Andrew Msechu (wa pili kushoto), pamoja na Mpigapicha Mkuu, Fielis Felix wakati wa mahojiano maalumu nyumbani kwake, Unguja Zanzibar, mwishoni mwa wiki. (Picha na Ofisi ya MKRZ)

Hatima ya SUK mikononi mwa Rais Samia

Na Waandishi WETU, Zanzibar

TIMU ya waandishi wa gazeti la Pambazuko ilitua kisiwani Unguja na kufanya mahojiano ya kina na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Katika mahojiano hayo – katika mfumo wa swali na jibu, Othman, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT-Wazalendo, alieleza mambo mengi likiwemo suala la chama hicho kudhamiria kujiondoa kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Endelea...

Pambazuko: Umepita muda sasa tangu ACT-Wazalendo mtangaze dhamira yenu kujitua kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), mmefikia hatua gani katika hilo?

Othman: Ni kweli kuwa mwezi Machi mwaka huu, Chama kilifikia uamuzi wa kujitua kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, baada ya kutoridhishwa na utendaji wa mambo ambayo yali-

paswa kutekelezwa na serikali hiyo.

Pia hatujaridhishwa na yanayotendeka kwa sababu ni tofauti kabisa na tuliyokubaliana. Hakuna hata moja ambalo tulikubaliana lifanyike chini ya SUK ambalo limefanyika.

Kwa hiyo tumeona kuendelea kubaki humo wakati kile kilichokubaliwa kufanyika hakifanyiki, ni sawa na kupoteza muda.

Baada ya kueleza dhamira ya kujitua tulikwenda kwa Mhesihimwa Rais Hussein Mwinyi na kumweleza dhamira yetu hiyo na kumpa sababu kwa nini tumefikia uamuzi huo.

Yeye alitupa ahadi zake ambazo hazajitekeleza.

Baada ya hapo tukaenda kwa Rais Samia Suluhu Hassan, naye ametupa ahadi zake ambazo muda wake wa utekezaji bado haujatimia.

Hivyo tunasubiri tuone yeye atafanya nini.

Pambazuko: Sasa hivi Zanzibar imetulia kwa sababu kuna SUK, je, ACT-Wazalendo haina hofu kuwa kujitua kwenye kunaweza kuirudisha Zanzibar kwenye siasa za uhasama?

Othman: Utulivu huu si kwamba kumetulia, utulivu huu ni wa kimya. Pita maeneo yote waulize watu wote, kila mtu sasa hivi ana wasiwasi kwamba mwakani tutakuwa na hali gani.

Kwa hiyo sasa hivi ni kimya, lakini kila mtu ana wasiwasi nini kitatokea mwakani wakati wa uchaguzi.

Inaendelea Uk. 18



Ana kwa Ana

Hatima ya SUK mikononi mwa Rais Samia

Inatoka Uk. 17

Pambazuko: Kwa hiyo Zanzibar ni kama bomu linalosubiri kulipuka?

Othman: It is true (ni kweli). Tunashangaa kuwa watu tuliowapa dhamana wakati tumetoka kwenye madhara ya 2015 na 2020, wanafanya mambo ambayo yanaweza kuturudisha tena kwenye hali kama ile. Madhara tumeya-document (kuyarekodi) vizuri.

Tumewawezesha sisi viongozi wote wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar wakutane siyo na sisi tu viongozi, bali tumewapeleka mpaka kwa waathirika na wakawaeleza kinagaubaga madhila waliyoyapata na kuyapitia.

Wao wenyewe wamesikia na kujionea jinsi watu walivyoathirika na yale yaliyotokea 2020.

Kuna watu ambao hawajawasikia hawa waathirika, lakini kama umewasikia na kuwona, hauwezi kuwa kiongozi mwenye ubinadamu kweli halafu usitake kufanya mabadiliko.

Sisi tulipoingia kwenye SUK, lengo letu la kwanza lilikuwa ni confidence and trust building (kujenga uamunifu na matumaini), yaani kujenga imani kwa watu kuwa huko mbele tunakokwenda tunakwenda kuweka hali ya amani.

Kwamba tufanye mambo yetu kwa utulivu, tuchague viongozi tunaowataka kwa amani na utulivu, bila ya udanganyifu na kuzua yale yaliyotokea 2020.

Pambazuko: Lakini Zanzibar inaelekea kati hali kama hiyo wakati wewe ni Makamu wa Rais ambaye moja ya majukumu yaliyokuweka madarakani ni kuhakikisha kuwa hayo haya-tokei. Unaifurahiaje kazi yako katika mazingira kama hayo?

Othman: Niseme wazi kabisa kuwa kwa kazi yangu kama Makamu wa Kwanza wa Rais sina

ile job satisfaction (kuridhishwa na kazi).

Hii ni kwa sababu tulipoingia tuliingia kwa malengo ya kurejesha hali ya amani na utulivu, jambo ambalo halijafanikiwa.

Tulipoingia hatukuingia kwa maana ile ya kujenga mabarabara, kujenga nini, tunajua hilo si tatizo la msingi la Zanzibar.

Lakini, niseme kuwa kinachonipa amani ni kuwa nami nimo na ninashiriki kwenye hizo juhudi za kutafuta hali nzuri kwa ajili ya Zanzibar.

Hili linanipa amani kwa sababu ninashiriki kwa nia njema na kwa juhudi.

Na katika kutimiza majukumu hayo, hakuna mtu ambaye sisi (ACT-Wazalendo) hatujazungumza naye. Hao watu wa CCM, wazee, wastaa-fu, kila mtu.

Nia yetu imekuwa ni ya dhati kwamba kwa nini Zanzibar tusifike mahali ambapo tunafanya uchaguzi ambao hautaumumiza mtu yeyote?

Mbaya zaidi ni kuwa kufanya uchaguzi huru si suala linalohitaji mabilioni ya fedha, inahitaji tu dhamira ya kweli.

Hawa wenzetu (CCM) haya ni mambo waliyoahidi kuyafanya lakini hawajafanya. Wamekwama wapi? Hakuna anayejua.

Pambazuko: Historia inaleta picha ya kuwa kila mara uchaguzi Zanzibar haujawa huru na haki. Ikitokea haya mnayoyadai yakatimizwa na uchaguzi ukawa huru na wa haki na chama kingine kikashinda. Mtakuwa tayari kukubali?

Inaendelea Uk. 19



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,
Othman Masoud Othman.

Hatima ya **SUK** mikononi mwa Rais Samia

Inatoka Uk. 18

Othman: Hilo tumelisema muda wote. Maa-lim Seif alilisitiza hilo. Tumeshasema kuwa tut-ampongeza yeyote atakayeshinda katika ucha-guzi ulio huru na wa haki, hatuna shida na hilo.

Tupo tayari si tu kukubali, bali kuwapongeza na kushirikiana nao. Kama tumeweza kushirik-iana nao katika mazingira kama haya, tutash-indwaje kushirikiana nao wakati wa amani.

Labda watu hawajui tumekwenda mbele ki-asi gani katika suala la kuifanya Zanzibar iwe na amani.

Sisi kipaumbele chetu wala si kushinda uch-aguzi. Kipaumbele chetu ni kuifanya Zanzibar iwe na amani.

Tunafanya hivi kwa sababu tunatambua kuwa Zanzibar haiwezi kutoka hapa ilipo kama tutaendelea na siasa za aina hii.

Kwa hiyo hata sisi tukishinda, kama mazin-gira yataendelea kuwa haya haya, ushindi wetu hautakuwa na maana yoyote.

Zanzibar sasa hivi ipo kwenye tope. Inabi-di kufanya juhudi za kuiondoa kwanza kwenye tope, ikae vizuri ndio inaweza kusonga mbele. Tukiendelea hivi wakati tupo kwenye tope, tut-aishia kuchafuana tu na hatutapiga hatua yoy-ote.

Pambazuko: Unauzungumziaje utawala wa Rais Mwinyi?

Othman: Nimekuwa kwenye utumishi wa umma kwa miaka mingi kabla ya kuja huku, miaka 25. Na nimekuwa kwenye nafasi nyingi nyeti ndani ya serikali ambako kati ya mambo nimekuwa exposed (niliyojifunza) ni miiko.

Moja na mambo ambayo tumekatazwa, ambayo watu wengi sasa hivi hawayazingatii hadi tumeingia kwenye uchawa, ni kum-profile (kumwelezea) mtu, kwa wema au kwa ubaya. Ni kitu ambacho kusema kweli hakitakiwi.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akizungumza na Mwandishi Mwandamizi wa Pambazuko, Andrew Msechu katika mahojiano maalum. (Picha na Fidelis Felix)

Pambazuko: Vipi kuhusu zile harakati za ki-siasa za hivi karibuni kutaka kumwongezea Rais Mwinyi muda wa kukaa madarakani?

Othman: Ukiziangalia kauli zile ni dhahiri kuwa hazikuwa za Chama Cha Mapinduzi, ile si position (msimamo) ya Chama Cha Mapinduzi.

Chama Cha Mapinduzi hakikuanzisha kile kitu, inaonekana ni watu ndani ya Chama Cha Mapinduzi ndio walifanya vile.

Kwa hiyo, sisi hatukuichukulia kauli ile kama jambo rasmi.

Lakini tukirudi kwenye msingi wa jambo hilo ni muda wa urais, hili ni suala la Kikatiba. Ni suala la Katiba na Katiba si mali ya chama. Chama hakiwezi kuamua mtu akae muda gani madarakani.

Chama ni mtoto wa Katiba, hivyo hakiwezi kuwa juu yake. Chama nacho kinatakiwa kui-heshimu Katiba.

Na kwa upande wa Zanzibar, kile kifungu kinachohusu muda wa rais kukaa madarakani kimelindwa. Hauwezi kukibadilisha mpaka uje kwa wananchi kuwauliza, wapige kura kama hili linawezekana au la.

Inaendelea Uk. 20

Ana kwa Ana

Hatima ya SUK mikononi mwa Rais Samia

*Rais Samia Suluhu Hassan***Inatoka Uk. 19**

Wanaosema hivyo walikuwa wanajifurisha, ni hali ya juu ya uchawa, hawakuwa na uwezo wa kutimiza hilo walilolitaka.

Pambazuko: Ndani ya SUK, je, mmefanya nini kama serikali kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana.

Othman: Kweli kuna mambo tumeyafanya. Lakini tatizo la msingi la kukosa ajira Zanzibar ni nini? Mimi naona tatizo ni jinsi tunavyoweza vijana.

Kwa mfano, leo Zanzibar tuna hoteli zaidi ya 600, lakini kuna mambo ya ajabu ajabu. Miaka 60 bado tunanunua wheel barrow (toroli), sepetu, tishu (karatasi laini za kujifutia), vijiiti vya kuchokonolea meno kutoka nje ya nchi. Hivi vyote tunanunua kutoka nje.

Tuna eneo kubwa la kubadilisha, tungeweza jambo, badala ya kununua kutoka nje tukatengeneza hapa na soko liko kubwa ndani na nje ya nchi.

Tulichotarajia ni kuweka mkazo kwenye uwekezaji mkubwa. Wapo watu wameanza, wana viwanda vidogo vidogo wanatengeneza tissue na vitu vidogo vidogo.

Inabidi sasa kuwa na programu za kuwainua hawa ili nao waweze kuwashika mkono wengine.

Kuna vijana wanafuga, lakini kuna matatizo ya msingi ambayo wanahitaji mitaji.

Kuna fish processing (kuchakata samaki). Nimetembelea Pemba kuna mtu amewekeza dola milioni 100, anahitaji takriban dola milioni 300 ili aweze kuimarisha shughuli zake asafirishe bidhaa nje.

Tumeweka mfuko wa uwekezaji. Tumejenga VETA. Ni juhudi tulizochukua, lakini mimi naamini bado hatujawekeza vya kutosha.

Pambazuko: Labda tatizo ni kuwa imezoeleka Zanzibar ni uchumi wa huduma. Serikali inafanya nini kubadili kutoka uchumi wa huduma na kuwa uchumi wa uzalishaji?

Othman: VETA ni moja ya solution (suluhisho). Lakini yule akitoka VETA anahitaji uwezeshaji. Tuna mfuko wa uwezeshaji, lakini hela inayokwenda kule ni ndogo sana.


Ukweli uchumi wa huduma wanufaika ni wachache. Tunahitaji mfumo ambao utawafaidisha wengi.

Chukulia mfano wa Mauritius. Wameanzaisha usajili wa kampuni offshore. Sharti lao moja kubwa ni kuwa kila kampuni inayosajiliwa lazima iajiri angalau raia watatu wa nchi ile. Sasa hivi Mauritius inafanya vizuri.

Naamini kuna njia tumechukua lakini zinahitaji msukumo mkubwa.

Inaendelea Uk. 21

Habarika kidijitali! Soma gazeti la **Pambazuko** na magazeti mengine maarufu kwenye **Rifaly!**



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com

Inatoka Uk. 20

Pambazuko: Je, mkazo ukiwekwa kwenye uchumi wa buluu tunaweza kufanikiwa?

Othman: Uchumi wa buluu tumewekeza watu wamepewa maboti, wapo wanaolima mwani, lakini mwisho wa siku tukubali kuwa tulichofanya tumerasimisha artisal fishing (uvuvi mdogo) zaidi. Vile vifaa walivyopatiwa haviwawezeshi kwenda mbali zaidi.

Lakini hata hapo wanapofika wakirudi na samaki unawafanyaje? Kuna utaratibu wa kumtenga samaki ili uweze kumsafirisha nje.

Tunapaswa kuwasaidia watu kwenye maeo kama hayo ili kukuza biashara ya nje pia.

Lakini kwenye uchumi wa buluu pia ni lazima muwe wazuri katika conservation (uhifadhi). Kama mkiacha kila mtu aende akavue samaki vile anavyotaka, mtaharibu eco system (mfumo wa mazingira).

Kuna eneo kubwa kwenye uchumi wa buluu la uzalishaji wa chumvi nadhani hatujalipa umuhimu mkubwa.

Hivyo ni kweli kuna fursa nyingi na kubwa kwenye uchumi wa buluu.

Pambazuko: Vipi una mpango wa kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar kwenye uchaguzi mwakani? Na upande wa Jamhuri, vipi mipango kuhusu kuungana na vyama vingine kama ilivyokuwa Ukawa?

Othman: Nikianza hili la Ukawa, ni fikra nzuri wakati ule ilipokuja na kwa kweli ilisaidia licha ya changamoto ilizokuwa nazo.

Sisi ACT-Wazalendo tunaamini tutakaposhirikiana itakuwa faida kwa chama chetu na wanchi kwa sababu tunachotafuta ni mageuzi ambayo tutayapata kwa urahisi tukishiriakiana.

Wapo ambao tunazungumza nao, lakini vipo vyama na sote tunajua kuwa vina stake (nafasi) kubwa kwenye uchaguzi, sasa pengine kwa mazingira wanayopitia kwenye siasa ni mape-ma kwao kusema kuwa tutaelekea wapi.

Hivyo tunawasubiri wakitulia, lakini sisi tunatumaini katika mashirikiano yenye tija.

Kwa upande wa Zanziabar mimi siwezi kujisemea mwenyewe kwa sababu chama kina taratibu zake za kumpata mgombea.

Tunachosema sasa hivi ni kuwa ni muhimu kuongoza hizi harakati na sasa hivi mimi ndiye

Hatima ya SUK mikononi mwa Rais Samia

kiongozi.

Itakapofika mahali wenzangu wakiwa na utashi wa kuona kuwa mimi ndiye ninayefaa kuwavusha kwa kuwa mgombea rasmi, basi watasikilizwa.

Wapo ambao tayari wameeleza utashi wao kwa hilo, lakini hilo bado halijanifanya niwe mgombea.

Na wala halijanifanya kuwa na uhakika kuwa mimi ndiye mgombea. Lakini mara zote wenzako wanapokuonyesha imani, ni vizuri kuwarudishia imani.

Pambazuko: Kwa nini hauwi muwazi katika hilo kwa sababu sifa ulizozitaja unazo, uwezo unao, watu wengine wameonyesha kuwa wanakuamini. Kilichobaki hapa ni dhamira yako. Wewe una dhamira ya kugombea?


Othman: Mimi misingi inayoniongoza ni kuwa wenzako wanakuonaje. Ifike mahali waseme kuwa unatufaa.

Mimi najijua kuwa natosha, lakini hiyo hai-toshi. Lakini pia mfumo tuliojiwekea mnafika mahali wenzako ndio wanasema wewe unafaa, lakini ukianza kusema mimi nafaa, nadhani hapo unaanza kutengeneza tatizo.

Itaendelea wiki ijayo...



Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi



Kenya

Utajiri mawaziri wa Ruto watisha



Rais wa Kenya, William Ruto

Inatoka Uk. 12

Kiongozi wa mawaziri ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Nje, Musalia Mudavadi, alitangaza thamani yake kuwa ni zaidi ya Shilingi za Kenya bilioni nne (sawa na Shilingi za Tanzania bilioni 82) inayotokana na umiliki wa nyumba za kifahari katika kaunti za Nairobi na Vihiga pamoja na mali nyingine.

Waziri mpya wa Madini na Uchumi wa Bahari, Hassan Joho, ambaye aliwahi kuwa Gavana wa Mombasa, alitangaza utajiri wake wa Shilingi za Kenya bilioni 2.3 (sawa na shilingi za Tanzania bilioni 47) akisema inatokana na umiliki wa kampuni kadhaa zikiwemo za kukusanya taka miongoni mwa mali nyingine. Joho anatoka kambi ya upinzani.

Aden Duale, mmoja wa marafiki wa Rais Ruto aliyerudi kwenye baraza, aliweka bayana utajiri wake kwamba unaotokana na kujishu-

ghulisha na kilimo na nyumba za kupangisha, unaofikia thamani ya Shilingi za Kenya milioni 980 (zaidi ya Shilingi za Tanzania bilioni 20).

Aliyekuwa mwanasheria mkuu ambaye sasa ni Waziri wa Utumishi, Justin Muturi, ana thamani ya Shilingi za Kenya milioni 801 (sawa na Sh16 bilioni), wakati waziri mpya wa elimu, Julius Ogamba, ana utajiri wa Shilingi za Kenya milioni 790 (takribani Shilingi za Tanzania bilioni 15).

Kithure Kindiki ambaye amerudishwa kwenye Wizara ya Usalama wa Ndani alisema utajiri wake unaotokana na kampuni yake ya uwakili na kwamba ukwasi wake ni Shilingi za Kenya milioni 694 (takribani Shilingi za Tanzania bilioni 14).

Waziri mpya wa michezo, Kipchumba Murkomen, amekiri kuwa na mali zenye thamani ya Shilingi za Kenya milioni 550 (sawa na Shilingi za Tanzania bilioni 11) ambazo amesema zinatokana na kumiliki majumba na magari.

Mawaziri wengine ambao thamani yao ni zaidi ya Shilingi za Kenya milioni 500 (Shilingi za Tanzania bilioni 10) inayotokana na umiliki wa nyumba za kukodisha na mashamba maeneo mbalimbali ya Kenya ni Wycliffe Oparanya, Opiyo Wandayi na Davis Chirchir.

Hali ikoje Tanzania?


Pamoja na kwamba sheria za Tanzania haziwabani mawaziri na viongozi wengine waandamizi kutangaza utajiri wao hadharani, wanatakiwa kuorodhesha mali zao kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Sheria inaeleza kuwa moja ya kazi ya sekretarieti hiyo ni kupokea taarifa za mali na madeni zinazohitajika kutolewa na viongozi wa Umma, hata hivyo, bado ni vigumu kuwabana “kutaja kila walichonacho.”

Ni kutokana na hali hiyo, viongozi wengi wa umma huficha umiliki wa mali na madeni waliyonayo- wengi wakiorodhesha mali chache mno kinyume na hali halisi.

Inaendelea Uk. 23

Je wajua



Kucha za mkono unaoutumika zaidi hukua haraka kuliko mkono ambao hautumiki, mfano kama unatumia mkono wa kulia basi kucha za mkono huo zitakua zaidi kuliko za mkono wa kushoto ndivyo hivyo kama unatumia mkono kushoto zaidi basi kucha za mkono huo zitakua haraka.



Ada Lovelace ni programa wa kwanza duniani. Na ndiye aliyetabiri kompyuta zitakuwa na uwezo mkubwa kuliko 'kalkuleta'.

Utajiri mawaziri wa Ruto...

Inatoka Uk. 22

Mazingira ya maisha ya familia za mawaziri na viongozi wengine wa umma, yanathibitisha hilo, kwani huiishi na kuonekana “kuogelea kwenye utajiri mkubwa.”

“Wewe unashangaa utajiri wa mawaziri wa Kenya, hapa Tanzania ni kufuru, wapo mawaziri wana majumba London (Uingereza) na hata Marekani, lakini hatujui, kwani wanaweka ukwasi wao mahali kwa siri kubwa,” amesema Dkt. Ibrahim Khalid, mchumi na Mkurugenzi wa IK Energies, ya Dar es Salaam.

Anasifu utaratibu wa viongozi wa umma wa Kenya kutangaza mali zao hadharani na kusailiwa na bunge kabla ya kuapishwa, akieleza kuwa unaweka uwazi wa umma kutambua viongozi wao wana utajiri wa kiasi gani.

Upo uwezekano mkubwa kwamba utajiri wa viongozi wengi waandamizi wa Tanzania wakamiliki fedha taslimu, mali na madeni mengi zaidi kuliko wenzao wa Kenya.

Hilo liliwahi kuthibitishwa na aliyekuwa Mbunge wa Bariadi Magharibi, Andrew Chenge ambaye ilibainika mwaka 2008, kwamba alikuwa akimiliki akaunti ya benki yenye kiasi cha dola za Marekani milioni moja.

Kiasi hicho, ambacho sasa ni zaidi ya shilingi bilioni 2.7, kilikuwa kimehifadhiwa

kwenye benki moja ndani ya Kisiwa cha Jersey.

Chenge alikutwa na kiasi hicho cha fedha baada ya kuanza kwa uchunguzi wa kashfa ya rushwa kwenye ununuzi wa rada uliowahusu maofisa waandamizi wa Tanzania na Kampuni ya BAE Systems iliyouza kifaa hicho.

Baada ya kubainika Chenge kuwa na kiasi hicho na kubanwa zaidi na waandishi wa habari kueleza namna alivyopata kiasi hicho kikubwa cha fedha alijibu; “ninyi kwanini mnahangaika na mimi na hivi vijisenti?”

Dkt. Ibrahim anasema kauli ya Chenge – akiwa mhitimu wa Chuo Kikuu cha Havard, Marekani, ambaye aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, bado inabeba maana kubwa na huenda wapo mawaziri wa Tanzania wenye utajiri kuliko wenzao wa Kenya.



Musalia Mudavadi



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Afande tukio la binti aliyedhalilishwa akamatwe

WIKI iliyopita, zilisambazwa picha za video za kikatili zilizokuwa zikiwaonyesha vijana fulani wakimdhali binti mmoja mwenye umri wa miaka 17.

Picha hizo za video ni kati ya picha mbaya zaidi kuangalia, kwa sababu tukio lenyewe lilikuwa ni la kikatili na udhalilishaji wa hali ya juu ambalo haliwezi kuvumiliwa hata kidogo.

Hakika, vijana hao waliokuwa wakionekana kufurahia ukatili huo, wanastahili adhabu kali kwa mujibu wa sheria wakipatikana na hatia, ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia za kinyama kama hizo.

Hata hivyo, mwishoni mwa wiki iliyopita, Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Mwandamizi wa Polisi, David Misime, aliuambia umma kwamba jeshi hilo limefanikiwa kuwatia nguvuni watuhumiwa wanne kati ya sita waliopanga na kutekeleza uhalifu huo.


Misime pia aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Clinton Honest Damas ambaye ni maarufu kwa jina la Nyundo, Playgod Edwin Mushi, Amin Lord Lema pamoja na Nikson Idala Jakson.

Aidha, msemaji huyo wa Jeshi la Polisi, alisema wamefanikiwa kuwakamata watu wengine wanne kwa kosa la kusambaza picha za ukatili huo kupitia mitandao ya kijamii.

Aliwataja watu hao kuwa ni Frora Mlombola, Aghatha Mchome, Madatha Jeremiah Budodi na James Nyanda Paulo.

Pamoja na hayo, Misime alisema katika taarifa hiyo, kwamba jeshi hilo linaendelea kuwasaka watuhumiwa wengine wawili ambao sasa wananchi wameombwa na Jeshi la Polisi, kutoa ushirikiano ili wakamatwe kwa haraka.

Hakika, Jeshi la Polisi linatakiwa kupongez-



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Mwandamizi wa Polisi, David Misime.

wa na kutiwa moyo ili kila anayefanya uhalifu akidhani hawezi kufikiwa na sheria, ajue anaweza kutiwa nguvuni wakati.

Wakati hayo yakiendelea, kilichobaki sasa ni jeshi hilo kuongeza kasi ya kuwasaka waliobaki akiwamo afande mmoja ambaye aliombwa msamaha na binti huyo kama sehemu ya kukiri makosa yake akiwa analazimishwa na watuhumiwa hao.

Afande huyo ambaye haijulikani kama ni miongoni mwa watuhumiwa wawili ambao wanaendelea kutafutwa, ni muhimu akamatwe na kuwekwa wazi katika tukio hilo kwa kuwa kuna kila dalili, kwamba ndiye aliyeratibu utekelezaji wa unyama huo.

Pamoja na watuhumiwa wengine kukamatwa na kutajwa kwa majina, bado wananchi kupitia mitandao ya kijamii wanahoji mahali alipo afande huyo ambaye inasemekana kuwa kiini cha ukatili huo.

Ni vyema sasa afande huyo asiakamatwe na umma umtambue, asiashwe aendeleo kula na kunywa kama alivyozoea kwa sababu ya uafande wake, bali asakwe popote alipo na kukamatwa.

Wananchi wanasubiri kwa hamu kumtambua na kuona aliyeitwa afande anafikishwa mbele ya vyombo vya sheria na haki ipatikane kwa binti ambaye amedhalilishwa kwa kiasi kikubwa.

Na Marché Arends

CHAMA cha African National Congress (ANC) cha Afrika Kusini sasa kinapumua. Ni baada ya kuchukua uamuzi mgumu wa kumtimua aliyekuwa kiongozi wake, Jacob Zuma (pichani).

ANC kilifikia uamuzi huo wa kuachana na Zuma, kutokana na sababu mbalimabli, kubwa ikielezwa kuwa ni “kwenda kinyume na misingi ya chama hicho.”

Itakumbukwa kuwa Zuma ambaye aliwahi kuwa Rais wa Afrika Kusini; 2009 hadi 2018, chama chake hicho kilimkigia kifua - kwa kiasi kikubwa hasa alipokumbwa na kashfa nzito zikiwamo za rushwa, kukwepa kodi, ubadhirifu na ubakaji.

Kamati ya nidhamu ya ANC, iliamua kumvua rasmi uanachama Zuma (82) kuwa kuwa aligeuka kuwa “muasi wa mingi” ya chama hicho.

Zuma hakutaka kujiondoa kwenye uanachama wa ANC, hata baada ya kuwa mwanzilishi wa uMkontho we Sizwe -kwa maelezo kwamba “hataondoka kwenye chama alichokisimamia,” lakini chama hicho kilichotawala Afrika Kusini baada ya kukoma kwa ubaguzi wa rangi, kikaona “anakitania na kufanya uhuni.”

“Hivi inawezekana vipi ukawa kiongozi wa chama kingine cha upinzani, na bado ukiwa mwanachama wa ANC? Viongozi wengi na hata wachama wa kawaida walikuwa wakihoji, huku wakitaka chama hicho kimtimue Zuma.

Wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita - Mei, mwaka huu, Zuma hakushughulika na ANC na akaweka wazi kuwa anafanya kila awezalo kuhakikisha uMkontho we Sizwe inashinda.

Katika uchaguzi huo, ANC ilipoteza umaarufu wake na hata kukwama kuunda serikali baada ya kuambulia asilimia 40 ya matokeo ya kura zote.

Chama kipya cha Zuma, Umkhonto we Sizwe, kilitajwa kuwa na mchango mkubwa kuporomoka kwa ANC, hasa katika maeneo ya Kwazulu.

Umkhonto we Sizwe kilipata asilimia 14.58 ya kura zote zilizopigwa na kukifanya kuwa chama cha tatu kwa ushindi mkubwa nchini humo.

Katika maoni yake kwa The Continent, kaimu msemaji wa ANC, Zuko Godlimpi alisema kuwa Zuma alikuwa na uhuru wa kuchagua kuendelea kuwa ndani ya chama chake zamani au kuondoka,

ANC sasa kupumua Zuma aking'olewa

lakini hakutaka kufanya hivyo hadi alipofukuzwa.

Godlimpi alinukuriwa akisema katika kipindi chote za Zuma kuonekana akishabikia chama chake cha uMkontho we Sizwe, hakuwahi kushtakiwa rasmi kwa kukiuka kanuni za chama.

Alisema hata baada ya Zuma kufukuzwa, bado hadi mwishoni mwa wiki hakuwa amewasilisha barua ya kukata rufaa ili kupinga uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya ANC kumfukuza.

Zuma alikuwa na siku 21 za kumruhusu kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo.

Makala haya ya uchambuzi, yamechapishwa kwa mara ya kwanza na The Continent, gazeti linalosambazwa kwa njia ya WhatsApp na kuchachapishwa kwa lugha ya Kiingereza. Unaweza kupata nakala yake bure, kila wiki kwa kujiandikisha kupitia namba hii ya WhatsApp; +27738056068





Wanyama wakikatiza kwenye ushoroba wa Kwakuchinja.

Chem Chem kulinda ushoroba Manyara

Mussa Juma, Babati

SERIKALI imesaini mkataba wa kulindwa eneo la mapito ya wanyamapori (ushoroba) la Kwakuchinja, ambalo lipo kati kati ya hifadhi za taifa za Tarangire na Ziwa Manyara.

Hatua hiyo itasaidia kuzuia uvamizi wa eneo hilo na kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu.

Mkataba huo umesainiwa wiki iliyopita Mjini Babati kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Wanyamapori na Taasisi ya Chem Chem.

Akizungumza baada ya mkataba huo kusainiwa, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Manyara, Fajra Ngerageza alisema ushoroba huo “utatunzwa kwa nguvu zote kutokana na umuhimu wake.”

Ngerageza alisema ushoroba wa Kwakuchinja una manufaa makubwa ya kiuchumi kwa Mkoa wa Manyara na taifa, hivyo lazima utunzwe na kulindwa.

“Sisi Mkoa wa Manyara, tayari tumekamilisha taratibu zetu za kuhifadhiwa ushoroba huo, ili kuendelezwa kwa shughuli za uhifadhi na utalii na tayari eneo limepimwa na mipaka yote imewekwa,” alisema.

Ngerageza alisema Mkoa wa Manyara unaendelea kutoa elimu kwa wananchi ambao wanaiishi jirani na eneo hilo kufanya shughuli ambazo ni rafiki kwa uhifadhi na utalii.

Ofisa Wanyamapori Mkoa wa Manyara, Felix Mwasenga alisema eneo hilo lina kilomita 137 za

ushoroba.

Mwasenga alisema eneo hilo limo ndani ya vijiji vya Vilima Vitatu, Kakoi, Minjingu na Olasiti.

Hata hivyo alisema katika eneo hilo, asilimia 20.9 lipo katika vijiji na asilimia 116 lipo katika hifadhi ya jamii ya Burunge.

Awali, akizungumza wakati wa kusainiwa mkataba huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Wanyamapori, Eligi Kimario alisema mkataba huo umesainiwa wakati muafaka ili kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu katika eneo hilo.

Kimario alisema ushoroba huo unaohifadhiwa utakuwa ukiruhusu wanyamapori kuvuka kutoka Hifadhi na Tarangire na kwenda Hifadhi ya Manyara bila kusababisha migogoro.

Alisema kumekuwapo na migogoro katika eneo hilo hasa baada ya baadhi ya wananchi kujenga nyumba na kulima eneo la mapito ya wanyamapori. Mkurugenzi huyo msaidizi alisema katika mkataba huo, Taasisi ya Chem Chem inatarajiwa kuwajengea uwezo watendaji wake kuhusu masuala ya uhifadhi na ushoroba huo.

Katibu wa Taasisi ya Chem Chem, Charles Sylvester alisema watahakikisha wanatekeleza matakwa ya mkataba huo kwa manufaa ya Tanzania na watu wake.

Alisema mkataba huo wa miaka mitano - na unaweza kuongezwa, utasaidia uhifadhi wa eneo hilo muhimu kwa sekta ya utalii na uhifadhi nchini.

Lissu, Mnyika, Sugu watiwa mbaroni

Inatoka Uk. 15

“Tunadai kuachiwa haraka na bila masharti viongozi, wanachama na wapenzi wetu wote waliokamatwa maeneo mbalimbali ya nchi. Chama kinafuafilia kwa makini yanayoendelea na kitaendelea kuuhabarisha umma kila linalojiri hatua kwa hatua,” alisema Mbowe.

Hali ilivyokuwa awali

Jana jioni, Tundu Lissu, baada ya kuwasili Mbeya kwenye kongamano na maandamano ya Bavicha kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani, alisema atahakikisha anashiriki kwenye shughuli zote zilizoandaliwa, licha ya Jeshi la Polisi kupiga marufuku.

Akizungumza muda mfupi baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege, Mbeya, Lissu alisema yuko tayari kukamatwa na kupelekwa gereza ni pindi atakapokuwa akishiriki maadhimisho hayo.

“Tuko hapa Mbeya kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani ambayo inatambuliwa kisheria, siyo katika nchi yetu tu, bali inatambuliwa kimataifa.

“Katika siku hiyo ya Umoja wa Mataifa, vijana hukutana ili kujadili mambo yanayowahusu na kuangalia namna ya kutatua changamoto zinazowakabili.

“Kwa hiyo, pamoja na kwamba Polisi wamezuia vijana wasiadhimishe siku yao, hiyo kesho (leo) hata kama nyinyi wengine mtakimbia, mimi nitaadhimisha peke yangu.

“Yaani, hiyo kesho (leo), aidha, tutasherekea au tutakuwa gerezani,” alisema Lissu ambaye alikuwa pamoja na Katibu Mkuu wa Chama hicho, John Mnyika.

Wakati Lissu akitoa msimamo huo, Jeshi la Polisi, lilikuwa limetangaza kuzuia shughuli zote zilizoandaliwa na Bavicha kwa maelezo kwamba “kulikuwa na viashiria vya uvunjifu wa amani.”

Katika taarifa yake kwa umma iliyotolewa jana na kusainiwa na Kamishna wa Oparesheni na Mafunzo, Makao Makuu ya Polisi, Dodoma, Awadhi J. Haji, Jeshi la Polisi lilisema kongamano la vijana wa Chadema lilizuiwa kwa kuwa

vijana hao walijipanga kufanya vurugu ili kusbabisha uvunjifu wa amani.

“Jeshi la Polisi limechukua uamuzi huo baada ya viongozi mbalimbali wa Chadema kuwahamasisha vijana kote nchini kwenda Mbeya ili kuungana na kuweka hatma ya Tanzania.

“Miongoni mwa kauli hizo ambazo zin-aashiria kuwa na lengo la kuvunja amani ni za Katibu wa Bavicha Taifa, Twaha Mwaipaya aliyekuwa akisema kama kijana yeyote unapenda nchi yako ya Tanzania, umeshalia miaka yako yote, siku hiyo ya tarehe 12/08/2024 tunakwenda kuweka hatma ya taifa letu Tanzania mkoani Mbeya.

“Kwa hiyo, kijana yeyote popote ulipo Tanzania, njoo Uwanja wa Ruanda Nzovwe, Mbeya.

“Tupo serious (makini) sana na jambo hili vijana wote wa Chadema kama ambavyo vijana wa Kenya wamejitambua, tunakwenda kuacha uteja wa serikali, vijana wa Kitanzania na kuweka maazimio makubwa ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025,” ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya Jeshi la Polisi.

Wakati huohuo, jana jioni kulisambaa taarifa na picha zikionyesha baadhi ya vijana waliotambulishwa na vyombo vya usalama, kuwa ni wanachama wa Chadema, wakiwa chini ya ulinzi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Chadema kilisambaza taarifa kwa umma kulaani kukamatwa kwa vijana hao na kutaka waachiwe mara moja kwa kuwa hawajafanya kosa lolote.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alisema katika taarifa yake kwamba chama chake kinalaani kitendo cha Jeshi la Polisi kuwakamata vijana wa chama chao.

Mrema alisema hadi jana saa 11 jioni, vijana wa Chadema walikuwa wamekamatwa katika vituo mbalimbali vya polisi nchini.

Alivitaja vituo hivyo na idadi ya vijana walioshikiliwa katika mabano, kuwa ni Temeke (11), Mbeya (10), Kituo Kikuu cha Polisi Iringa (104), Migori Isimani, Iringa (35), Makambako, Njombe (74) na Mikese, Morogoro kulikuwa na vijana 48.



Riwaya

Viaticum

Sakramenti ya Mwisho



Na Mchungaji Godwin Chilewa, Texas. Marekani

MWAKA 1990 kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Baba Mtakatifu Yohane Paulo wa Pili, alifanya ziara ya kihistoria nchini Tanzania.

Ziara hiyo iliyoonekana kuwa ya kawaida kwenye macho ya wengi, ilisifiwa na mamilioni ya watu kwa kuchochea imani na upendo kwa watu wa imani na dini zote duniani.

Miaka zaidi ya 30 baadaye, ndipo inapobainika kuwa ziara hiyo haikuwa ya kawaida kama wengi walivyofikiri; bali ilikuwa na ajenda nyingine kubwa na ya siri kuu.

Siri inayoweza kusambaratisha kanisa katoliki duniani, na kusababisha umwagaji mkubwa wa damu ya watu wasio na hatia.

Alihitajika mtu mwenye nguvu na ujasili wa kuzima moto huo kabla haujakolea kiasi cha kufanya maangamizi.

Katika giza nene lililotanda kila mahali, mwandishi wa habari za uchunguzi, kepteni Eddy Kashe bila kujua anaingizwa kazini kuutafuta ukweli uliofichwa kwa zaidi ya robo karne. Ukweli unaolindwa kwa gharama ya damu za

watu.

Muhimu: Majina yote na matukio ndani ya riwaya hii ni ya kufikirika;

Endelea...

Sura ya Kwanza

Ilikuwa imeshatimia saa tatu na nusu asubuhi, muda ambao kwa kawaida humkuta kepteni Eddy Kashe akiwa kwenye pilikapilika nyingi. Lakini siku hii ilikuwa ya tofauti sana.

Pamoja na kusoma barua pepe zote, na kupitia kitabu chake cha kumbukumbu za kila siku, bado hakuona jambo lolote la kusiimua.

Akanyanyua simu yake ya mkononi kuangalia kama kuna ujumbe wowote ulioingia muda huo, lakini pia hakuona chochote cha maana. Siku hii ilianza bila makeke kabisa.

Kama ungemuona asubuhi hii bila shaka ungempenda kwa jinsi alivyoumbika kiume hasa; mrefu kiasi cha futi sita inchi moja, siyo mnene wala siyo mwembamba.

Mwili wake ulijengeka vyema kutokana na mazoezi ya nguvu aliyofanya tangu alipokuwa mdogo na hasa alipokuwa jeshini.

Uso wake wa duara na macho ya ujanjaujanja, ulificha umri wa miaka thelathini na mbili alionao. Ngozi yake ya maji ya kunde, nywele nyeusi, na sharubu zilizochongwa vyema, vilikuwa kivutio kikubwa kwa mabinti wa mjini ingawa yeye hakuwa mwingi wa habari.

Asubuhi hii alivalia shati jeupe, suruali ya kijivu na viatu vya ngozi nyeusi vilivyotengenezwa na Bruno Magli.

Kwa muda aliendelea kuchokonoa simu yake akiperuzi mitandao ya kijamii hadi alipokinai, akairudisha mezani.

Akavuta faili moja kati ya manne yaliyowe kwa upande wa kushoto wa meza yake, akalifungua, akalikodolea macho kwa sekunde chache. Halafu ghafla, kama mtu aliyekumbuka kitu fulani akalifunga.

Akanyoosha mkono wake wa kulia akavuta gazeti la Mizani lililokuwa kwenye mtoto wa meza, akalitandaza mezani. Akarudia kusoma habari iliyoandikwa kwenye ukurasa wa mbele.

Jana majira ya saa tano na dakika ishirini asubuhi, majambazi wenye silaha walimuua kwa

Inaendelea Uk. 29



Viaticum

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

kumpiga risasi Mwenyekiti wa Bodi ya Mafuta ya Petroli (TPDC), Brigedia Jenerali mstaafu Shabani Nyoni na walinzi wake wawili, Sajenti Abdallah Kombo na Koplo John Didi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Watu wengine wanne walijeruhiwa vibaya na kukimbizwa hospitali ya Muhimbili, Dar es Salaam. Taarifa kutoka makao makuu ya Jeshi la Polisi zimeeleza kuwa, majambazi hao walivamia Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), City Branch na kupora shilingi milioni 300 za ki-Tanzania, dola 25,000 za ki-Marekani na hazina mbalimbali za wateja zilizohifadhiwa kwenye visanduku binafsi.

Jeshi la Polisi linaendesha msako mkali kuwatafuta wahalifu hao. TPDC imetangaza zawadi ya shilingi milioni 50 kwa yeyote atakayetoa taarifa zitakazosaidia kukamatwa kwa majambazi hao. Eddy alimalizia kusoma sentesi ya mwisho huku akitingisha kichwa kwa masikitiko.

Hii ilikuwa mara yake ya tano kusoma habari hii, lakini kila alipoisoma ilimchoma moyo kana kwamba ilikuwa ndiyo mara yake ya kwanza.

Tukio lenyewe lilitokea siku mbili zilizopita na kuandikwa kwenye gazeti la siku iliyofuata. Hata hivyo, kwa Eddy habari hiyo iliendelea kuwa kama mpya kila wakati.

Katika maisha yake, Brigedia Nyoni alishika nyadhifa mbalimbali serikalini ikiwa pamoja na katibu mkuu kiongozi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na mshauri wa rais wa mambo ya usalama.

Kabla ya kuteuliwa kushika nafasi za kisiasa Brigedia huyo alikuwa mkuu wa brigedi ya Faru ya JWTZ.

Eddy alikuwa na uhusiano wa kipekee sana na brigedia huyu aliyezoea kumuita kwa jina la utani 'Gorong'ondo.'

Wakati alipokuwa kwenye mafunzo ya awali

ya ukomando huko 92KJ Ngerengere, Brigedia Jenerali Nyoni wakati huo akiwa luteni kanali, ndiye aliyekuwa mkuu wa kikosi. Makomando wote walimheshimu na kumpenda sana.

Hata alipoondoka 92KJ, Eddy aliendelea kuwa na mawasiliano ya karibu na kama huyo aliyemchukulia kama mzazi na kuwa mshauri wake wa karibu.

Mawasiliano yalipungua baada ya Nyoni kuachana na kazi za operesheni za jeshi na kujikita zaidi kwenye majukumu ya kisiasa akiwa mmojawapo wa washauri wa rais wenye nguvu zaidi.

Jambo lililomshitua na kumkera zaidi Eddy ni kule kuongezeka ghafla kwa matukio ya uhalifu mkubwa nchini.

Hili lilikuwa tukio la tatu katika kipindi cha mwezi mmoja. Wiki tatu kabla ya tukio hili, waziri wa sheria na katiba aliuawa kwa kupigwa risasi na kuporwa gari lake aina ya Toyota Landcruiser na siku kumi baada ya hilo afisa mwandamizi wa Idara ya Usalama wa Taifa anayesimamia operesheni za kificho, bwana Magnusi Lime akauawa kwa kupigwa risasi na kuporwa gari lake aina ya BMW X1 xDrive 28i.

Tukio hili lilisababisha mshituko mkubwa zaidi kwa sababu majambazi hao walimvamia ofisa huyo mchana kweupe, tena akiwa kwenye maegesho ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, sehemu yenye ulinzi wa kuaminika kabisa.

Matukio haya yalimumiza kichwa kwa sababu kwa uzoefu wake, Eddy alijua fika kwamba majambazi hupenda kufanya uhalifu kimyakimya na kutoweka bila kuua ili kupunguza msukumo wa askari kuwatafuta.

Kinyume chake, majambazi hawa walikuwa wakiua bila sababu jambo lililomfanya ahisi waliikuwa wakituma ujumbe kwa serikali au kundi la watu fulani.

Itaendelea toleo lijalo...



Habari

Masoko Dar hatari kwa afya

Na Hellen NGOROMERA

AFYA za wakazi wa Jiji la Dar es Salaam zimo hatari ni baada ya kubainika kukithiri kwa uchafu unaorundikana katika masoko.

Waliomo kwenye hatari zaidi ni wafanyabiashara ndani ya masoko hayo, wanunuzi wa bidhaa na huduma pamoja na wafanyakazi wengine.

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko kwa zaidi ya wiki umebaini kuwa baadhi ya masoko hayo haya-na miundombinu mizuri, mifumo na vifaa vya kukusanya, kuhifadhi, kuchakata na kusafirisha taka ngumu na laini.

Katika soko la Ilala Boma, Manispaa ya Ilala, Pambazuko limeshuhudia kuwepo mrundikano wa uchafu unaosababisha harufu mbaya na kutapakaa kwa inzi.

Sehemu kubwa ya mitaro ya kupitisha maji machafu imeziba, huku maji hayo yakizagaa katika mae-neo ambayo hupangwa bidhaa - nyingi zikiwa ni za vyakula.

Pambazuko lilishuhudia maji hayo machafu yanayotoka katika mitaro yakitiririka jirani na bidhaa zinazouzwa sokoni hapo kama mboga, matunda na aina nyingine ya vyakula.

Kutokana na uchafu huo, mazingira ya soko hilo yanatoa harufu mbaya pamoja na kuwa na hewa nzito jambo ambalo linahatarisha afya za wafanyabiashara pamoja na wengine wanaokwenda sokoni hapo.

Akizungumza na Pambazuko sokoni hapo, Mwanaidi Said, ambaye alikwenda kwa ajili ya kununua mahitaji, alisema hali ya usafi sokoni hapo hairidhishi na akabainisha kuwa kutodhibitiwa kwa uchafu kunaweza kusababisha milipuko ya magonjwa, kama kipindupindu.

Ayubu Ayubu alisema mazingira ya uchafu sokoni hapo yanaonyesha namna viongozi wanaopewa dhama-na ya kusimamia uendeshaji wa soko “wanavyojisahau.”

Hali ni ya kuridhisha kidogo katika Soko la Buguruni na baadhi ya watu waliozungumza na gazeti hili walikiri kuwa hali hiyo ni nzuri kidogo kulinganisha na siku za nyuma.

Maeneo mengi ya soko hilo yalionekana yakiwa katika mpangilio mzuri, kwani hata bidhaa zinazopangwa chini zimetengewa eneo maalum.

Siku za nyuma, hasa wakati wa mvua mazingira ya soko hilo yalikuwa katika hali mbaya kutokana na kuzungukwa na uchafu mwingi na matope hali ambayo ilikuwa adha kwa wafanyabishara ya wateja.

Jitihada za mwandishi wa gazeti hili kuzungumza na uongozi wa soko zilishindikana kwani walikataa kusema chochote kwa maelezo kuwa watazungumza tu baada ya kupata ruhusa kutoka kwa viongozi wao wa juu kutoka Manispaa.

Katika Soko la Kariakoo, hali ni mbaya hasa kwenye eneo la udhibiti wa taka ngumu, ingawa kwa upande wa taka laini mitaro yake inapitisha maji vizuri, hata hivyo, nyakati za mvua inazidiwa.

Hivi karibuni, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Mkama Bwire, alikiri mfumo wa majitaka katika eneo la Kariakoo kuwa chakavu, na kuahidi kurekebisha.





Na Hellen
NGOROMERA



Fahamu kinachosumbua ndoa nyingi

HABARI wasomaji wangu wa safu ya uhusiano. Ni mtarajio yangu kuwa mmeianza wiki vizuri na mpo salama na mnaendelea vyema na shughuli zenu za kila siku.

Tuendelea na suala la ndoa kwa sababu suala hili ni pana sana na lina mambo mengi ndani yake. Ni muhimu tukaendelea na mada ya ndoa kwa sababu ni msingi wa kujenga familia bora.

Leo nitazungumza namna matendo maovu ya mke au mume yanavyoweza kufifisha, kuharibu au kuvunja ndoa au uhusiano.

Ni wazi kwamba mume na mke huungana pamoja kwa lengo la kuanzisha familia yenye furaha na maendeleo.

Wawili hao wanapofunga ndoa ama kuamua tu kuishi wakiwa mume na mke, huona fahari kuanza maisha mapya katika hali ya furaha, kwani kila mmoja hupata hamu ya kumwonyesha upendo mwenzake.

Lakini wapo wachache ambao huipata raha hiyo kwa muda mfupi tu.

Kiuhalisia, maisha ya ndoa hutakiwa kuwa ya furaha, amani na upendo kati ya wawili hao na pia ndugu na jamaa.

Hata hivyo, maisha ya ndoa nyingi siku hizi

yamekuwa tofauti, kwani asilimia kubwa ya ndoa huvunjika muda mfupi baada ya ndoa kufungwa.

Ndoa nyingi zimevunjika kutokana na wawili hao kushindwa kuvumiliana, kuwekeana visa-si na hata gubu.

Nimeshuhudia ndoa ya rafiki yangu wa karibu ikidumu kwa mwaka mmoja tu! Chanzo ni mwanamke kushindwa kuvumilia tabia za mumewe!

Rafiki yangu alinidokeza kwamba tangu aolewe alikuwa na furaha ya ndoa kwa miezi miwili pekee.

Alisema mumewe alikuwa akitumia muda mwingi nje ya nyumbani, akakosa kumjali, kumthamini, huku akimweleza hakuna alichojali.

Vikao vya usuluhishi vilifanyika bila mafanikio, akachoka akaamua kutengana naye!

Mara nyingi wanaume huwa chanzo kikuu cha migogoro ya ndoa, hali inayosababisha wake zao kuchoka na kuamua kutengana nao.

Wanaume wengi huwanyanyasa wake zao kihisia mara nyingi bila ya wao kujua. Mwanamke ni mtu wa hisia sana, hivyo ili aweze kudumu kwenye ndoa, mwanamume anatakiwa kujali sana hisia za mkewe.

Wanawake ni wavumilivu wa hali ya juu katika vitu mbalimbali na unapooni mwanamke aliyeolewa kavunja uhusiano wake na mumewe, ujue kwamba amefanya uamuzi kwa moyo mguumu sana.

Kikubwa ninachohimiza hapa ni kuwa wanandoa wana wajibu wa kupendana kwa dhiti na kuheshimiana katika misingi iliyo bora.

Wanaume wana wajibu mkubwa wa kuwapenda, kuwatunza wake zao na kuwaona wana thamani kubwa katika maisha yao.

Kutangatanga kwa wanaume huku na kule na kuwapa maumivu wake zao, kunaweza kuziweka familia katika mahangaiko na taabu nyingi.

Kikubwa ninachoshauri wanandoa ni kubaki katika maisha waliyoamua na kama kuna sintofahamu, wawekane sawa na kusonga mbele.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

'Lips' zako zinahitaji kutunzwa hivi

HALI ya hewa inaweza kuathiri sehemu mbalimbali za mwili wako hususani midomo.

Majira ya baridi ndiyo hasa ambayo husababisha midomo kukauka ama kukatika.

Hii hutokea kwa baadhi ya watu wasiopendelea kutumia njia bora za kuweka unyevu kwenye 'lips' kama vile kutumia mafuta ya mgando.

Leo nimekuwekea matumizi ya asali na unga wa manjano kama kilainishi cha lips zako.

Mahitaji

*Asali kijiko kidogo kimoja

*Unga wa manjano kijiko kidogo kimoja.

Changanya mahitaji yako vizuri kisha chukua kitambaa chenye maji, pangusa midomo yako. Jisugue kama unafanya 'scrub' kwa muda wa dakika mbili, kisha nawa na maji ya uvuguvugu.

Kisha upake 'lipbalm' au mafuta ya mgando. Fanya hivyo kila unapopata nafasi.

Kisha upake 'lipbalm' au mafuta ya mgando. Fanya hivyo kila unapopata nafasi.



Unaujua mfuko mdogo wa jinzi uliokosa kazi maalumu?

KAMA ni mvaaji wa suruali za jinzi utagundua kuwa kuna mfuko mdogo juu ya mfuko wa kawaida upande wa kulia.

Je, umewahi kuutumia ama kujua ulitengenezwa kwa matumizi gani?

Leo nakujua kupitia safu hii kuwa mfuko huo mdogo ulianza kutumika miaka ya 1890 ukiwekwa maalumu kwa ajili ya kutunza saa.

Hapo zamani saa zilizotumika zilikuwa ni zile za kushika mkononi au unaning'iniza na cheni ndogo kiunoni au shingoni, hivyo ili kupata namna bora ya kuzihifadhi.

Kampuni ya kwanza kutengeneza jinzi ya Levis iliweka mfuko huo ambao umekuwa ukiwekwa hadi leo kwenye jinzi zinazotengenezwa na kampuni tofauti.

Kwa miongo mingi sasa, mfuko huo hautumiki tena kuhifadhi saa na wala hauna matumizi sahihi, kwani wapo ambao huchomeka fedha za sarafu au noti ama wakati mwingine, huwekwa kitu chochote kidogo ili kuhifadhi kwa wakati huo kisipotee.



Afcon 2024



Nani akabidhiwe utamaduni Pamoja Afcon 2027?

Na John MARWA

MOJA ya maeneo muhimu ya kutazama wakati ambapo Tanzania, Kenya na Uganda zikiwa mbioni kuhakikisha zinaandika historia ya kuandaa michuano mikubwa ya kandanda Afrika; Pamoja Afcon 2027, ni eneo la utamaduni.

Kwamba nchi tatu hizo ambazo zimekabidhiwa dhamana ya kuandaa michuano hiyo ya soka, zinajiandaa nini kuonyesha utamaduni wa maeneo yao kwa wageni?

Afrika Mashariki ni eneo lenye makabila mengi, mila zinazotofautiana na pengine kushabihiana kwa kiasi, lakini nini hasa kifanyike kutambulisha eneo hilo?

Siku chache zilizopita, dunia ilishuhudia - katika kilele cha "Simba Day," meneja wa habari na mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, akitumia utamaduni wa Kabila la Masai kuingia uwanjani, jambo ambalo lilikuwa kivutio kikubwa.

Haikuwa tu kuburudisha, bali kuuza na kutangaza utamaduni wa Kimasai ambao wanapatikana Tanzania na Kenya, hasa katika maeneo ya bonde la ufa.

Kwa namna alivyopangilia Wamasai kumsindikiza, ilionyesha ubunifu ambao unaweza kuigwa.

Wakati ambao maandalizi ya Pamoja Afcon 2027, yanazidi kupamba moto, basi nchi hizo wenyeji zisisahau kuuza utamadauni wake.

Ukweli ni kwamba Tanzania pekee ina makabila zaidi ya 120, Kenya wana makabila yasiyopungua 44, lakini ni Wamasai ndio wamekuwa alama ya Wakenya kama utambulisho na utalii wa kitamaduni licha ya kuwepo ukabila katika taifa hilo.

Uganda ni taifa ambalo pia lina makabila yasiyopungua 40, kabila maarufu zaidi katika taifa hilo ni Baganda, wapo pia Wajie ambao ukwatazama mavazi yao yana utambulisho unaoendana na Wamasai.

Wajie ni kabila la watu linaloishi katika milima ya kaskazini mashariki mwa Uganda. Lugha yao ni lahaja ya Kikaramojong, ambayo ni kati ya lugha za Kiniloti ambayo ndio lugha ya jamii ya Wamasai wa Tanzania na Kenya.

Kwa jumla, wanahusiana sana na majirani wao, Wakaramojong upande wa kusini na Wadodoth upande wa kaskazini. Ni wazi hawa ni alama ya kipekee katika taifa hilo.

Ikiwa Tanzania, Kenya na Uganda hakuna taifa lililojipambanua katika alama ya utamaduni wao, vazi la mataifa yao, sasa ni wasaa wa kuwaandaa hawa ndugu zetu katika picha kubwa ya kuitambulishia dunia utamaduni ambao unaweza kubainisha utamaduni wao kwa pamoja.

Yawezekana wakawa Wahaya, Wakurya, Wachaga na Wazaramo, ama tuseme ni Wakisii, Wajaruo na Wakikuyu labda wawe Waganda, Wanyoro, Wakiga, Waatooro, Wafumbira, lakini nani atavutia zaidi ya Wamasai?



Na Mwandishi wetu

INAFIKIRISHA kifo cha utata cha msanii wa kizazi kipya Bongo Fleva, Joseph Francis, maarufu kwa jina la Mandojo kilichotokea Jijini Dodoma kwa kupigwa na wananchi waliodhania kuwa ni mwizi.

Msanii huyo amefariki jana wakati akipatiwa matibabu kutokana na majeraha aliyoyapata katika moja ya hospitali jijini humo.

Chanzo cha kifo

Mandojo anadaiwa kuondoka nyumbani asubuhi Agosti 11, 2024, baada ya kugombana na mke wake na hakurejea nyumbani, na baadaye alitafutwa na marafiki zake bila mafanikio.

Siku hiyohiyo, kulisambaa video kwenye mitandao ya kijamii, ikionyesha Mandojo akiwa amezingwa na kundi la watu “wakimshushia kipigo” baada ya kudaiwa kuwa mwizi.

Taarifa hizo ni kwa mujibu wa rafiki wa Mandojo, Msafiri Yera ambaye ndiye aliye kwenda Kituo cha Polisi kuripoti tukio hilo na baadaye kumpeleka hospitali ili atibiwe majeraha.

Salamu za rambirambi

Akituma salamu za rambirambi, Naibu Waziri Utamadauni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma almaarufu - Mwana FA ameandika kwenye ukurasa wake wa X; “Habari mbaya sana. Hata sina cha kusema. Tumeporwa mtu mzuri sana, na mwanamuziki fundi hasa. Pumzika kwa amani ndugu yangu “Dojo”. Naamini wahusika wanafahamu kuwa hatua zinawafuata”

Naye Diamond Platnumz ameandika; “Hii ni habari ya kusikitisha, pumzika kwa amani, mshindi” kupitia mtandao wa Instagram.

Msanii Roma Mkatoliki ameandika; “Eeeh! Baba, Pumzika Mwanangu Dojo, Hii imetumiza wengi sana” kupitia mtandao wa X.

Enzi za uhai wake, Mandojo alitamba na ‘ngoma’ kama vile Nikupe nini, Dingi, Muziki Chacha na nyingine nyingi akiwa na mwanamuziki mwenzie, Domo Kaya.


Mandojo:

Nyota iliyozima kama mshumaa

Tetesi za Usajili



Olympiki 2024



Tah

Beki wa kati, Jonathan Tah kutoka Bayer 04 Leverkusen, bado hajabadilisha mawazo yake ya kujiunga na Klabu ya FC Bayern Munich, huenda dili hilo likachochewa na kuondoka kwa beki Matthijs de Ligt.

Mawissa



Klabu ya AS Monaco imekamilisha dili la kumsajili beki wa kati Christian Mawissa kutoka Klabu ya Toulouse kwa kandarasi ya miaka mitano. Vipimo vya afya vya mchezaji huyo kufanyika hivi karibuni.

de Ligt, Mazraoui

Klabu ya Manchester United imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa kati Matthijs de Ligt pamoja na beki wa pembeni, Noussair Mazraoui kutoka Klabu ya FC Bayern Munich kwa kandarasi ya miaka mitano.



Mshindi wa medali ya dhahabu katika mbio za mita 200, Letsile Tebogo.

Yuko wapi Tebogo wetu?

Na Mwandishi WETU

TANZANIA inashindwa nini katika michuano ya kimataifa kwenye michezo? Nani ameiropa nchi hiyo iliyokuwa na sifa kubwa, hasa katika riadha na masumbwi.

Yuko wapi Letsile Tebogo wake? Yeye amewezaje, nani kamshika mkono, je, ni ulozi, rushwa ana matumizi ya dawa za kuongeza nguvu?

Tebogo, mwanariadha wa Botswana mwenye miaka 22 tu, amewezaje kuwa kinara wa mbio za mita 200 na kutwaa dhahabu, huku Tanzania ikikosa medali hata moja?

Iko wapi sifa ya Tanzania kuwa kinara kwenye michano ya Olimpiki, Jumuia ya Madola na mingine?

Je, Tanzania hakuwa vijana wenye uwezo, je, hakuna utashi wa viongozi, je, ni nini hasa kinakwamisha kurejea kwa sifa za Tanzania kwenye riadha?

Hakika maswali ni mengi, ambayo hayana majibu ya haraka kutoka kwa wahusika wenye dhama ya kusimamia michezo.

Sifa ya Tanzania kuwa kinara wa mbio ndefu duniani, imezimwa rasmi jana, baada ya wanariadha wake wawili; Magdalena Shauri na Jackline Sakilu kukosa medali yoyote.

Wanariadha hao wameungana na wenzao sita – wote wakiambulia patupu, ambao walikuwa Paris, Ufaransa kwenye mashindano ya michezo ya Olimpiki mwaka huu ikifanyika Paris, Ufaransa.

Kuanzia jana, imetimu miaka 40 tangu Tanzania itwae medali kwenye mashindano hayo.

Katika mbio za jana – upande wa wanawake, wawakilishi hao wa Tanzania walishindwa hata kuwakaribia washindi ambao ni Mholanzi Sifan Hassan aliyeibuka mshidi na kufuatiwa wa na Muethiopia, Tigst Assefa na Mkenya Hellen Obiri.

MICHEZO

Jumatatu, Agosti 12 - 18, 2024



Hivi Yanga hii inafungwaje?

Na Mwishishi WETU

SWALI kubwa – la kimichezo, hivi sasa nchini Tanzania ni moja tu; “hivi Yanga hii inafungwaje?”

Hilo ni swali linaloulizwa maeneo mengi, siyo mijini tu, bali maeneo mengi ya nchi ambako kuna mashabiki na wafuatiliaji wa kabumbu.

Pamoja na kwamba jibu lake linategemea majibu ya mtu mmoja mmoja, lakini jana tena, Yanga imed- hihirisha kuwa ni timu kubwa na ngumu kufungika, baada ya kuibamiza Azam FC mabao 4-1.

Timu hizo zilikutana kwenye mchezo wa fainali ya Ngao ya Jamii katika dimba la Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Kocha wa Azam, Yousuph Dabo, itabidi ajilaumu mwenyewe kwa kushindwa kuiheshimu Yanga kwa kupunga mfumo wa walinzi watatu ambao walirahi-

sisha kazi ya viungo washambuliaji mahiri wa Yanga, na kufunga magoli matatu ya haraka haraka.

Tangu kuanza kwa mchezo huo, Yanga ilionekana kucheza vizuri huku pasi ndefu zikionyesha wazi ud- haifu wa mabeki wa pembeni wa Azam.

Hata hivyo, ilikuwa ni Azam iliyopata goli la kuongoza katika dakika ya 13 baada ya mpira ulio- okolewa na mabeki, kumkuta winga Gibril Silla am- baye alitoa pande kwa Feisal Salum aliyeubetua mpira huo na kumwacha golikipa wa Yanga, Djigui Diarra akishindwa kuudaka.

Baada ya goli hilo, Yanga ikaimarisha zaidi mfu- mo wao wa kupiga pasi ndefu na iliwachukua dakika tano tu kusawazisha baada ya moja ya pasi hizo iliy- opigwa na Mudathir Yahya kutoka mbele kidogo ya mstari wa kati wa kiwanja kumkuta Price Dube, am- baye msimu uliopita alichezea Azam, na kupachika goli la kusawazisha.

Dakika kumi baadaye, pasi nyingine ndefu ikam- kuta mlinzi wa kushoto wa Yanga, Shadrack Boca ambaye alikimbia na mpira na kupiga krosi kali iliy- sindikizwa wavuni na mlinzi wa kati wa Azam, Yoro Diaby, akausindikiza wavuni.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

